

**UKIUKAJI WA KANUNI ZA UPOLE KATIKA *MHANGA NAFSI YANGU***

**NA**

**GLADYS W. KINYUA**

**KAZI HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2015**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kingine chochote.

### **Mtahiniwa**

Gladys W. Kinyua

Sahihi: \_\_\_\_\_

Tarehe: \_\_\_\_\_

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika chuo kikuu cha Nairobi.

### Msimamizi

Dkt. Amiri Swaleh

Sahihi: \_\_\_\_\_

Tarehe: \_\_\_\_\_

### Msimamizi

Bw. Josephat Gitonga

Sahihi: \_\_\_\_\_

Tarehe: \_\_\_\_\_

## **TABARUKU**

Naitabaruku kazi hii kwa mume wangu Ashford Kinyua kwa kusimama name kipindi chote nilipokuwa masomoni. Namtabarukia baba yangu mpendwa kwa kuniombea na kunihimiza nikazane, watoto wangu purity, Edwin, Charles, Victor na mjukuu wangu Jeff kwa uvumilivu mwingi waliokuwa nao katika kipindi hicho cha masomo yangu.

## **SHUKURANI**

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa busara, uvumilivu na muda wa kukamilisha safari hii. Shukurani pia natoa kwa wasimamizi wangu Dkt. Amiri Swaleh na Bw. Josephat Gitonga. Ushauri wenu umenisaidia sana katika utafiti huu. Asanteni sana kwa uvumilivu wenu mlipokuwa mkirekebisha kazi yangu.

Namshukuru mwalimu Bw. P. Mwangi kwa usaidizi wako nilipokuwa naandika pendekezo la utafiti. Asante sana kwa muda wako mwingi ulitumia kunielekeza kila nilipokuhitaji.

Wahadhiri wengine katika chuo kikuu cha Nairobi asanteni sana kwa uelekezi wenu . Hawa ni pamoja na Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri na Prof. John Habwe. Mungu awabariki na awape nguvu na neema mnapowaongoza wengine. Namshukuru mume wangu Ashford Kinyua na watoto wangu Purity, Edwin, Charles, Victor na mjukuu wangu Jeff kwa uvumilivu wao kwa kipindi chote nilipokuwa nasoma. Mungu awabariki sana. Siwezi kuwasahau Bw. na Bi. Antony Nyaga kunipa motisha katika safari ya masomo yangu.

Ndugu na marafiki, asanteni sana kwa maombi yenu yaliyonipa nguvu kila siku. Mungu awarehemu nyote mlionisaidia kwa njia moja au nyingine katika masomo yangu.

## **YALIYOMO**

Ungamo.....	ii
Tabaruku .....	iii
Shukurani .....	iv
Yaliyomo.....	v
Iksiri .....	ix

## **SURA YA KWANZA**

1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Tatizo la utafiti .....	2
1.3 Maswali ya utafiti .....	3
1.4 Madhumuni ya utafiti.....	3
1.5 Sababu ya kuchagua mada hii.....	3
1.6 Upeo na mipaka .....	4
1.7 Maelezo ya istilahi .....	4
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada .....	4
1.9 Misingi ya nadharia .....	8
1.10 Nadharia tete .....	10
1.11 Njia za utafiti.....	11
1.11 Hitimisho.....	11

## **SURA YA PILI**

### **NADHARIA YA UPOLE NA UKIUKAJI WA UPOLE KATIKA MHANGA NAFSI**

#### **YANGU**

2.0 Utangulizi.....	12
2.1 Mitazamo ya Fraser (1990).....	12
2.1.1 Mtazamo wa upole kama mkataba wa mazungumzo .....	12
2.1.2 Mtazamo wa mazungumzo .....	13
2.1.3 Mtazamo wa kuhifadhi uso.....	13
2.1.4 Mtazamo wa upole kama kaida ya kijamii .....	16
2.2 Kanuni za ushirikiano za Grice.....	17
2.2.1 Kanuni ya Ubora.....	17
2.2.2 Kanuni ya Idadi.....	17

2.2.3 Kanuni ya Uhusiano.....	17
2.2.4 Kanuni ya namna .....	18
2.3 Kanuni za Leech (1983).....	20
2.3.1 Kaida ya mkakati .....	20
2.3.2 Kaida ya kujitweza.....	20
2.3.3 Kaida ya kumsifu msikilizaji .....	21
2.3.4 Kaida ya ukarimu .....	21
2.3.5 Kaida ya makubaliano .....	21
2.3.6 Kaida ya kumwonea huruma msikilizaji .....	21
2.4 Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) .....	22
2.4. Vitendo vinavyotishia uso.....	23
2.4.1 Njia za kukabiliana na vitendo vinavyotishia .....	23
2.4.2 Mkakati wa kuwa kwenye rekodi .....	24
2.4.2.1 Katika hali ya dharura au kutamauka .....	24
2.4.2.2 Katika kitendo cha kumfaidi msikilizaji.....	24
2.4.2.3 Kutoa ahadi kwa msikilizaji .....	24
2.4.2.4 Tofauti za kimamlaka kati ya msemaji na msikilizaji.....	25
2.5 Mkakati wa nje ya rekodi.....	25
2.5.1 Kutumia vidokezo.....	25
2.5.2 Kuzua utata .....	26
2.5.3 Kutumia kejeli/kinaya.....	26
2.5.4 Kutumia maswali ya balagha.....	26
2.5.5 Matumizi ya sitiari .....	26
2.6. Mkakati hasi wa upole .....	26
2.6.1 Kutumia maswali na vidokezi.....	27
2.6.2 Kutumia vitangulizi .....	27
2.6.3 Kuomba msamaha.....	27
2.6.4 Kuonyesha heshima baina ya msemaji na msikilizaji .....	27
2.6.5 Kutaja kanuni ya jumla .....	28
2.6.6 Kuwa bila rajua .....	28
2.7 Mkakati chanya wa upole .....	28

2.7.1 Kumtambua na kumshughulikia msikilizaji .....	28
2.7.2 Kutumia vitambulisho vya makundi.....	29
2.7.3 Kutafuta makubaliano.....	29
2.7.4 Kuepuka kutokubaliana .....	29
2.7.5 Kutumia ucheshi .....	29
2.7.6 Kuwa mrijua .....	30
2.7.7 Kuuliza au kutoa sababu za kitendo fulani .....	30
2.7.8 Mkakati wa kutotekeleza kitendo kinachotishia uso .....	30
2.8 Hitimisho .....	33

## **SURA YA TATU**

### **MATUMIZI YA LUGHA KATIKA *MHANGA NAFSI YANGU***

3.0. Utangulizi.....	34
3.1 Mbinu zilizotumiwa kujenga na kuendeleza maudhui katika <i>Mhanga Nafsi Yangu</i> .....	34
3.1.1 Uzungumzi Nafsi .....	34
3.1.2. Nyimbo .....	35
3.1.3 Misemo .....	36
3.1.4. Methali .....	38
3.1.5. Tanakali za sauti.....	38
3.1.6. Tashbihi.....	39
3.1.7. Kuchanganya Ndimi .....	40
3.1.8. Urudiaji .....	41
3.1.9 Mbinu Rejeshi.....	42
3.1.10 Ukiukaji wa kanuni za upole .....	43
3.2. Hitimisho .....	51

## **SURA YA NNE**

### **MAUDHUI KATIKA *MHANGA NAFSI YANGU***

4.0 Utangulizi.....	52
4.1 Sinopsia ya Mhanga Nafsi Yangu .....	52
4.2 Ukiushi wa upole unavyoendeleza maudhui katika <i>Mhanga Nafsi Yangu</i> .....	53
4.2.1 Wasiwasi .....	53
4.2.2 Matumaini .....	54

4.2.3 Maovevu na dhulma.....	57
4.2.4 Tuhuma .....	57
4.2.5 Udhalilishaji.....	58
4.2.6 Huzuni.....	59
4.2.7 Uozo wa jamii.....	60
4.2.8 Unafiki .....	61
4.2.9 Usaliti.....	62
4.2.10 Ubaguzi wa Rangi.....	64
4.2.11 Udhalilishaji.....	65
4.2.12 Majuto.....	67
4.3 Hitimisho .....	68

### **SURA YA TANO**

5.0 Utangulizi.....	71
5.1 Matokeo .....	71
5.2 Matatizo ya utafiti.....	72
5.3 Mapendekezo .....	72
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>73</b>



## **IKSIRI**

Upole ni suala muhimu sana katika kuanzisha na kudumisha mahusiano mema baina ya wanajamii. Ili kudumisha mahusiano hayo, wazungumzaji wakati wote hulazimika kutumia mikakati mbalimbali ya upole ili kuhifadhi nyuso zao na za wenzao. Tasnifu hii ni uchunguzi wa jinsi ukiushi wa kanuni za upole umetumiwa katika *Mhanga Nafsi Yangu* ili kujenga na kuendeleza maudhui. Uchunguzi huu ulinuia kubainisha iwapo ukiushi wa kanuni za upole katika riwaya hii umefaulu kujenga na kuendeleza maudhui makuu katika riwaya teule. Ulinuia pia kubainisha ni wahusika wapi wametumiwa kuendeleza maudhui makuu. Tulikusudia pia kuchunguza kama nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987, 1978) na kanuni za upole za Grice (1975) zinaweza kutumika kuchanganua kazi ya fasihi andishi.



## SURA YA KWANZA

### 1.1 Utangulizi

Katika mawasiliano, mtu huwa na jukumu la kuwasilisha ujumbe ambao unaeleweka. Katika shughuli nzima ya kuwasilisha ujumbe ni muhimu kuhakikisha ya kwamba ujumbe umewasilishwa kwa njia ifaaayo huku kanuni za upole zikizingatiwa. Ni muhimu katika mawasiliano yoyote mtu kuchagua maneno na hata njia mwafaka ya kuwasilisha ujumbe bila kumuudhi anayeupokea ujumbe huo.

Mawasiliano yoyote hutumia lugha fulani. Lugha katika mawasiliano huwa na majukumu mawili makuu ambayo ni;-

- i) Kuendeleza shughuli k.v za kibiashara
- ii) Shughuli ya kuingiliana kijamii

Kwa mujibu wa Levinson na Brown (1987, 1978) ambao ndio waasisi wa nadharia ya upole. Jukumu la kwanza la lugha na la muhimu huwa ni kufikisha ujumbe muhimu na kuafikia hatima ya jambo fulani k.m kama ilikuwa ni biashara, mteja na muuzaji wanaweza kuafikiana. Katika jukumu la pili muhimu huwa ni kudumisha uhusiano mwema katika jamii husika. Katika jukumu la pili, ni lazima mtu azingatie ni nani anazungumza naye kwa sababu si maneno yote yanaweza kutumiwa kwa mtu yeyote. Kuna jinsi watoto huwasiliana na watoto wenzao na jinsi wanavyowasiliana na watu waliowazidi umri.

Katika mawasiliano ni vizuri kuzingatia maadili ya jamii husika ili kuzingatia upole katika mazungumzo. Ili kuweza kuelewa ni mambo gani yanafaa kusemwa bila kumuudhi anayeambiwa ni vizuri kuzingatia mahusiano ya kijamii, matabaka na vyeo. Hii ni kwa sababu swala la upole ni la kijamii na kila jamii ina mtazamo wake wa upole. Kile ambacho jamii moja inachukulia kuwa upole kinaweza kuwa si upole katika jamii nyingine. Katika jamii, inatarajiwa kuwa mtu wa cheo cha juu anafaa kuzungumziwa kwa heshima zaidi akilinganishwa na mtu wa kawaida. Mawasiliano hutegemea pia kama ni rasmi au ya kirafiki. Jamii pia inachukulia kuwa tajiri anafaa kuzungumziwa kwa heshima zaidi akilinganishwa na maskini.

Kwa jumla, katika mawasiliano ni muhimu kuzingatia kanuni za upole ili kuhifadhi heshima ya anayezungumziwa. Anayepitisha ujumbe anafaa kuhakikisha kuwa ujumbe umewasilishwa bila

kumuudhi au kumwaibisha anayeupokea.

Utafiti huu ulinuia kuchunguza kama ukiushi wa kanuni za upole katika *Mhanga Nafsi Yangu* ya S.A Mohamed umesaidia kujenga na kuendeleza maudhui katika riwaya hiyo.

## **1.2 Tatizo la utafiti**

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu upole na umuhimu wake katika kuanzisha na kudumisha mahusiano katika jamii na hasa katika miktatha mbalimbali ya mitagusano ya kijamii. Hata hivyo, hakuna utafiti uliofanywa kuhusu swala la upole katika kazi ya fasihi andishi na hasa riwaya ya S.A. Mohammed *Mhanga Nafsi Yangu*.

Kama tulivyotangulia kusema, katika mawasiliano kuna umuhimu wa kumfikiria unayemzungumzia. Kwa mujibu wa wataalamu walioasisi nadharia ya upole, mtu ana nyuso mbili; uso chanya na uso hasi. Uso chanya hutaka kuhifadhiwa katika mawasiliano. Lazima anayezungumza ahakikishe kuwa anachosema hakitamuudhi anayesikiliza wala kumwaibisha. Msemaji anafaa kuchagua maneno yake vizuri ili kuhakikisha kuwa maana iliyolengwa ndiyo iliyowasilishwa.

Uso hasi huwa hautakiwi kujitokeza. Uso hasi hutaka kuwa huru na hutaki shughuli zake kuingiliwa. Hutaka kufanya mambo bila mtu kutaka kujua anafanya nini na kwa nini anafanya hivyo.

Kwa mujibu wa Grice (1975) ambaye amezungumzia upole kuna mambo muhimu ya kuzingatia katika mawasiliano. Mambo haya ndiyo yanayoitwa kanuni za ushirikiano za Grice. Kanuni hizi ni;

- i) Kiasi - katika mawasiliano msemaji asitumie maneno mengi ambayo si muhimu. alenge jambo ambalo anataka kusema tu.
- ii) Ubora - Kanuni hii inadai kuwa jambo litakalosemwa liwe ni ukweli ambao unaweza kuthibitishwa. Mtu asiseme uongo.
- iii) Uhusiano- Lazima unapozungumza ujihusishe na mada inayozungumziwa. Usichanganye mambo ambayo hayana uhusiano na yale yanayosemwa.
- iv) Namna au jinsi - Katika mawasiliano, lazima kinachosemwa kiwe wazi. Msikilizaji hafai

kutatizika katika kuelewa kinachosemwa.

Katika utafiti huu tumeangalia jinsi mwandishi amekiuka kanuni na mikakati ya upole iliyopendekezwa na Grice (1975) na Brown na Levinson (1978) kwa madhumuni ya kujenga maudhui na kuboresha kazi yake.

### **1.3 Maswali ya utafiti**

- i) Ukiukaji wa kanuni za upole unadhihirika katika kauli zinazotolewa na wahusika wakuu au wahusika wajenzi?
- ii) Ni mambo gani yanayochochea ukiukaji wa kanuni za upole katika Mhanga Nafsi Yangu?"
- iii) Ukikaji wa kanuni za upole umesaidia kuendeleza maudhui katika Mhanga Nafsi Yangu?
- iv) Nadharia ya upole inaweza kutumiwa kuchanganua kazi ya fasihi andishi?

### **1.4 Madhumuni ya utafiti**

Malengo ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza mambo yafuatayo;

- i) Ni wahusika wapi wanatoa kauli zinazokiuka kanuni za upole.
- ii) Ni mambo gani yanachochea ukikaji wa kanuni za upole katika *Mhanga Nafsi Yangu*
- iii) Kuchunguza kama ukiukaji wa kanuni za upole katika Mhanga Nafsi Yangu umesaidia kuendeleza maudhui katika riwaya hii.
- iv) Kuchunguza kama nadharia ya upole inaweza kutumiwa kuchanganua kazi ya fasihi andishi.

### **1.5 Sababu ya kuchagua mada hii**

Tulichagua kufanya kazi hii kwa sababu swala la upole halijashughulikiwa sana katika kazi ya fasihi na hasa katika kazi teule ya *Mhanga Nafsi Yangu*. Maswala ambayo yanashughulikiwa ni ya kijamii kama nafasi ya mtoto katika jamii, maudhui katika kazi nzima ya fasihi, maswala ibuka katika kazi za fasihi andishi, nafasi ya mwanamke katika jamii, utabaka na mengineyo.

Sababu nyingine ya kuchagua hii mada ni kuwa nadharia ya upole haijatumika sana kuchambua

kazi za fasihi andishi. Kazi nyingi za fasihi zilizochambuliwa hutumia nadharia kama za ufeministi, sosholojia, nadharia ya kimaksi na nyinginezo. Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kudhihirisha kuwa nadharia ya semantiki inaweza kutumiwa kuchambua kazi ya fasihi.

## **1.6 Upeo na mipaka**

*Mhanga Nafsi Yangu* ndiyo kazi tuliyoishughulikia. Tumechunguza ukiukaji wa kanuni za upole kwa mujibu wa waasisi wa nadharia ya upole Levinson na Brown(1978) na Grice (1975) na ni vipi ukiushi huu umesaidia kuboresha kazi nzima ya S.A Mohammed. Tumechunguza jinsi mwandishi ametumia lugha katika mawasiliano ya wahusika na pia katika usimulizi wake. Tumechunguza kama ukiukaji wa kanuni za upole umesaidia kuendeleza maudhui katika kazi teule na pia tumechunguza ukiukaji huo unachochea na nini.

## **1.7 Maelezo ya istilahi**

K.M - Kwa mfano

K.V - Kama vile

MDR - Mikakati ya ndani ya rekodi

MUC - Mikakati ya upole chanya

MUH - Mikakati ya upole hasi

MNR - Mikakati ya nje ya rekodi

Ukiushi - katika tasnifu hii ukiushi unarejelea matumizi ya lugha kwa njia isiyofaa.

Upole - Upole katika tasnifu hii unarejelea matumizi ya lugha kwa njia inayostahili

## **1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada**

Habwe (2010) ameshughulikia swala la upole katika karatasi yake "Swahili Forum 17 (2010) *Politeness Phenomena: A case of Kiswahili Honorifics* Katika kazi hiyo anasema kuwa jamii ya waafrika hupendelea matumizi ya upole wakati wa mawasiliano. Anasema kuwa upole husaidia kudumisha heshima kati ya watu wa vyeo mbalimbali katika jamii. Habwe anasisitiza kuwa lugha inayotumiwa na wakazi wa Nairobi hudumisha upole kinyume inavyoaminiwa kuwa mikakati ya upole haizingatiwi na wakazi hao. Anasema, kwa mujibu wa waasisi wa nadharia ya

upole hasa Leech (1983); Levinson (1983), Brown and Levinson (1978, 1987) upole ni namna ya kuokoa uso wa msikilizaji, ni utambuzi ambao mtu humwonyesha mtu mwingine kupitia kuepuka kaida au desturi fulani za mazungumzo. Habwe anaendelea kusema kuwa swala la upole ni swala lenye utata kwa sababu linahusu matumizi ya mikakati mbalimbali. Moja ya mikakati hiyo ni umri. Kwa mfano katika jamii ya waislamu ni watoto ambao husalimia wakubwa wao kwa kuwapa shikamoo. Mtoto akimpita mtu mzima bila kumpa shikamoo hiyo katika jamii ya waialamu ni ukiukaji wa kanuni ya upole. Jamii nyingi za waafrika pia hutarajia mtoto awaamkue na sio wao waanze salamu. Iwapo mazungumzo yataendelea, mtoto hafai kukatiza mazungumzo ya mkubwa wake na akifanya hivyo basi amekiuka kanuni za upole katika jamii. Uchunguzi wa Habwe unaonyesha kuwa matumizi ya maneno kama `tafadhali`, `pole`, `samahani` hutumika sana katika mazungumzo ya watu wa Nairobi. Matumizi ya maneno haya kwa kawaida huleta uhusiano mwema na upole huwa dhahiri.

Katika kazi hii, hambwe alikuwa anachunguza mikakati ya upole ambayo hutumiwa na watu wa Nairobi. Mikakati mingine inayotumiwa si ya moja kwa moja. Msemaji anaweza kutumia maswali badala ya kusema jambo moja kwa moja. Msemaji pia anaweza kutumia mikakati wa kujitweza ili kumfurahisha msikilizaji. Kwa mfano :

"mimi sikufikii katika upishi" au "Ningekuwa mwalimu mzuri kama wewe ningefurahi sana"

Habwe anasema kuwa matumizi ya mikakati ya upole kati ya wakazi wa Nairobi husaidia kuhifadhi uso wa msikilizaji. Watu wa Nairobi hujaribu kutumia mikakati ya upole wanapowasiliana katika hali ya kawaida.

Habwe (2010) katika *Nordic Journal of African Studies* 19(3) Dialogue Drama in Kenyan Political Speeches and its Pragmatic Implications ameshughulikia swala la upole akizingatia kanuni za upole za Grice. Grice (1975) alipendekeza kanuni nne za upole. Katika kazi hii ya Habwe amezingatia kanuni hizo za Grice(1975) na (1977). Katika kazi hii habwe alichunguza jinsi wanasiasa wa Mombasa na Nairobi wanavyotumia mikakati ya upole wanapohutubia umati wa watu. Anasema kuwa Kenya ni mojawapo ya mataifa ya Afrika Mashariki yanayotumia lugha ya Kiswahili. Ni taifa ambalo linaweka misingi yake kwa vyeo, kabila, dini, utamaduni na rangi. Uchaguzi nchini Kenya huongozwa kwa misingi ya kabila, dini na mambo mengine mengi. Si rahisi kuona mtu wa kabila fulani akipewa kura na watu ambao si wa kabila lake.

Kwa sababu ya misingi hiyo, siasa za Kenya huwa zimejaa mizozo na kila mmja hujaribu kuwashawishi wapiga kura na kuonyesha nguvu zao za kisiasa.

Ili kuweza kuwashawishi wapiga kura wanasiasa hutumia mikakati mbalimbali ili wawashawishi wananchi kuwapigia kura.

Katika kazi hii, Habwe alichunguza mikakati ya upole ambayo wanasiasa wa Nairobi na Mombasa hutumia ili kupata kura kutoka kwa wananchi.

Raitania (2014) katika tasnifu yake alishughulikia swala la upole. Alichunguza mikakati ya upole katika vipindi vya runinga na hasa Mawaidha na Bi Mswafari katika runinga ya Citizen. Kipindi hiki hupeperushwa na runinga ya citizen kikiwa ni kipiondi cha kutoa mawaidha kuhusu ndoa. Alieleza jinsi Bi Mswafari na watangazaji Kanze Dena na Lulu Hassan huendeleza kipindi hiki. Anaeleza jinsi mikakati ya upole imezingatiwa katika kipindi hiki.

Maviaka(2014) katika tasnifu yake alichunguza maswala ibuka katika *Mhanga Nafsi Yangu*.

Alichunguza jinsi maswala yanayoibuka katika riwaya hii yanavyoathiri wahusika. Kwa kuwa ametumia nadharia ya uhalisia amechunguza jinsi mambo haya hujitokeza katika hali halisia ya maisha.

Hakuna kazi yoyote iliyoandikwa kuzungumzia jinsi upole umekiukwa katika *Mhanga Nafsi Yangu* ya S. A. Mohamed. Hata hivyo kazi zilizofanywa kuhusu mawasiliano na matumizi ya lugha zimesaidia katika utafiti huu. Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa matumizi ya lugha hudhihirika katika muktatha maalum wa jamii na kuwa wakati wa mawasiliano ni muhimu kuzingatia muktatha. Katika kazi yetu tumechunguza ni vipi muktatha wa mawasiliano unaweza kuchochea matumizi ya lugha bila kuzingatia upole, hivyo maoni yao ni muhimu katika kazi yetu.

Trudgil (1983), anasema kuwa kila jamii ina sheria zinazoongoza matumizi ya lugha, mwingiliano na mtagusano wa wanajamii. Anasema kuwa katika mawasiliano, ni lazima mtu aelewe utamaduni wa jamii yake ili aweze kutumia lugha inavyotarajiwa. Ni lazima au ni muhimu kuelewa ni vipi mtoto anafaa kuongea na wakubwa wake ili asionekane kukiuka matarajio ya jamii husika. Katika kazi yetu tuliangalia kama matarajio ya jamii yamekiukwa katika mawasiliano ya wahusika katika *Mhanga Nafsi Yangu*.



Lackoff (1976) anahusisha lugha na vitengo vingine vya jamii kama ilivyo sayansi na kudai kuwa pekee haiwezi kujitosheleza. Mtalaam huyu anadai kuwa utafiti wowote wa kiisimu lazima ujikite katika kueleza sababu za watu kuongea jinsi wafanyavyo. Anadai kuwa maswala mengi katika lugha kama vile muktatha, sababu ya tamko au usemi fulani, jinsi ya kutafsiri usemi, upole katika usemi ni baadhi ya mambo ambayo hayajashughulikiwa sana.

Kulingana na Lackoff (1976), si sahihi kuzingatia sintaksia pekee katika matini na kupuuza muundo ndani wa tungo. Ni muhimu kujiuliza ni kwa nini mzungumzaji anazungumza jinsi afanyavyo. Anatoa kauli kuwa si sawa kuwa na uamuzi wa jumla kwamba kila binadamu mwenye akili razini lazima atumie njia fupi anapozungumza. Anasisitiza kuwa ukamilifu wa maana hutegemea alichokusudia msemaji. Hata kama anakubali kuwa si sawa kuwa na uamuzi wa jumla anakubaliana na mikakati ya upole ya Grice (1975).

Kazi hii imechangia pakubwa utafiti wetu kwa sababu baadhi ya mambo tutakayochunguza ni matumizi ya lugha kwa kuzingatia kanuni nne za mawasiliano za Grice (1975)

Wamitila (2003) anasisitiza umuhimu wa lugha katika mawasiliano. Msemaji au mwandishi anaweza kuathiri mawasiliano kama atatumia lugha vibaya. Anasisitiza kuwa matumizi ya lugha ni kipengele muhimu cha kuchanganua jamii inayohusika. Kauli hii ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu tutajaribu kuchunguza ni nini kilichomchochea S. A. Mohamed kutumia lugha inayokiuka kanuni na mikakati ya upole.

Guiner (1998) anaeleza jinsi lugha ilivyotumiwa kumdhalilisha kama mwanamke lakini hakufa moyo. Anaeleza kuwa alidhalilishwa na wanaume waliokuwa na taasubi ya kiume alipokuwa akisomea uanasheria. Wanaume walikuwa wanatumia lugha inayokiuka kanuni za upole kwa sababu hawakuwathamini wanawake. Kazi hii imesaidia katika uchunguzi wetu kuelewa ni kwa nini wahusika wengine katika "*Mhanga Nafsi Yangu*" walitumia lugha bila kuzingatia upole.

Guiner anathibitisha kuwa dhara inaweza kumfanya mtu kumzungumzia mwingine bila kuzingatia upole.

Guiner (1995) anasema kuwa hata kama alidunishwa kwa kuwa mwanamke alionyesha upole hata alipokuwa na tajriba kubwa kuhusu jambo fulani zaidi ya wenzake wanaume. Kwa kuwa kazi yetu inahusu ukiukaji wa kanuni za upole, tumechunguza kama udunishaji wa mhusika

mkuu akiwa Peponi ni baadhi ya vichocheo vya ukiukaji wa kanuni za upole katika *Mhanga Nafsi Yangu*.

Kupitia udurusu tuliofanya na marejeleo ya vitabu tulivyosomwa, ni dhahiri kuwa suala la upole katika mawasiliano halijatafitiwa katika *Mhanga Nafsi Yangu*.

### **1.9 Misingi ya nadharia**

Katika kazi hii tumetumia nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1978) na kanuni za ushirikiano za Grice (1975) Kamusi ya karne ya ishirini na moja inaeleza upole kama hali ya kuwa mtaratibu. Nadharia ya upole iliasisiwa na Stephen C. Levinson na Penelope Brown (1978). Nadharia ya upole inadai kuwa watu hutumia mikakati mbalimbali ili kuhifadhi uso wa msikilizaji. Kwa mujibu wa Levinson na Brown (1978), kuna uso chanya na uso hasi. Uso chanya hutaka kuhifadhiwa na kutambuliwa. Hii inamaanisha kuwa unapooonea na mtu, unafaa ujaribu usimuudhi au kumuabisha. Uso hasi huwa hautaki kuingiliwa. Mawazo na maoni yake huwa ni mwisho na ukijaribu kupinga au kurekebisha unamuudhi.

Kulingana na wataalamu hawa, iwapo kuna uwezekano wa kuathiri hisia za mtu ni lazima mtu atumie mikakati ifaayo katika mawasiliano. Mikakati atakayotumia itategemea uhusiano uliopo baina ya msemaji na msikilizaji. Nadharia hii inatambua mikakati minne ambayo mtu anaweza kutumia katika mawasiliano ambayo ni;

- i) Mikakati ya ndani ya rekodi.
- ii) Upole chanya.
- iii) Upole hasi.
- iv) Mikakati ya nje ya rekodi.

MDR hutumiwa wakati watu ambao wamezoeana wanazungumza. Watu hawa ni K.V marafiki, watu wa familia au watu wanaofanya kazi pamoja na mna urafiki wa karibu. Unapotumia MDR huwa hujihadhari sana kuhifadhi uso wa msikilizaji. Mikakati hii hutumiwa na watu ambao hutaniana.

MUC hutumiwa pale ambapo msemaji na msikilizaji wanajuana kiasi. Huwa msikilizaji na msemaji wanajuana lakini msemaji huwa makini asiadhiri au kuaibisha uso wake. Huwa

msemaji anajaribu kutambua cheo na nafasi ya msikilizaji katika jamii. Kwa mfano ikiwa umesahau simu yako nyumbani unaweza kumuomba huyo mtu simu yake bila kutatizika, ama iwapo unataka kununua kitu na umesahau pesa nyumbani unaweza kumuomba pesa bila kutatizika sana. Unaweza kumwambia mtu "Tafadhali nisaidie na simu yako nipige nyumani." Mtu ambaye mmezoeana na mnataniana unaweza kumwambia, "hebu lete hiyo simu yako nitumie kidogo."

MUH hutumika pale ambapo msemaji anajihisi kuwa anamsumbua anayesema naye. Unapotaka kuelezewa njia na mtu ambaye hamjuani itabidi umtahadharishe kwanza kuwa ungetaka kuongea naye k.m. "samahani unaweza kunielekeza njia ya kwenda kawangware.

MNR hutumika pale ambapo msemaji anataka jambo lifanywe lakini hasemi moja kwamoja k.m. badala ya kumwambia mume wako kuwa unataka kupelekwa nje kwa chakula cha jioni unaweza kusema "siku nyingi hatujaenda nje kwa chakula cha jioni."

Brown na Levinson (1978:66) wanasema kuwa dhana ya uso ilitokana na kazi ya Ervin Goffman (1959) na pia kutokana na tamko la kiingereza ambalo huchukulia "uso" kama dhana ya kuaibika au kutokuwa na uso mbele ya watu. Mtu anaposema kuwa hana uso mbele ya watu huwa anamaanisha kuwa ana aibu kubwa. Katika juhudi zao za kufafanua uso' waliasisidhana ya "uso chanya" na "uso hasi."

Lakoff na Johnson (1980) wakichangia kuhusu dhana ya uso wanadai kuwa "uso" ni sitiari ambayo hutumika kila wakati. Wanadai kuwa kila wakati katika mazungumzo ni lazima kukumbuka kuwa mtu ni lazima ajaribu asimuudhi, kumuaibisha au kutotambua nafasi ya mtu katika jamii. Jambo hili ni la kweli kwani hakuna wakati mtu huwa na nia ya kuudhi mwenzake katika mazungumzo ya kawaida. Dhana ya uso inaweza kutokuwa na maana pale ambapo watu wanateta au hawaheshimiani hata kidogo. Watu wanapoteta huongozwa na hisia za hasira na hivyo huwa vigumu kuzingatia upole.

Mtalaam mwingine ambaye alishughulikia mawasiliano na dhana ya upole ni Paul Grice (1975). Kulingana na Grice (1975) mawasiliano hukamilika kutokana na juhudi za msikilizaji na msemaji. Wote wawili wana jukumu la kuhakikisha ya kwamba mawasiliano yameendelezwa kwa njia ifaayo. Katika kazi yake "Logic and conversation" anasisitiza kwamba lazima pawe na makubaliano katika mawasiliano yoyote.

Katika kazi yake Grice alitoa kanuni nne ambazo ni muhimu katika mawasiliano. Kanuni hizi alizitaja kama;

- i) Kiasi
- ii) Ubora
- iii) Uhusiano
- iv) Namna

Kanuni ya kiasi inadai kuwa mzungumzaji atumie maneno kwa kiasi fulani na asiongeze maneno mengi ambayo hayaongezi maana kwa kile anachotaka kusema. Wakati mwingine mtu anaweza kuwa anasema kitu lakini kabla aseme awe amepita njia ndefu sana. Hali hiyo ndiyo hupelekea mtu kuambiwa "tafadhali fupisha kauli yako".

Kanuni ya ubora inasema kuwa katika mawasiliano sema jambo ambalo unajua ni ukweli kiasi kwamba unaweza kuthibitisha.

Kanuni ya uhusiano inadai kuwa unapozungumza ujihusishe na mada inayozungumziwa. Usichanganye mambo ambayo hayahusiani na yale yanayosemwa. Hata hivyo kanuni hii inaweza kukiukwa iwapo mtu anataka kujiepusha na yanayozungumziwa

Kanuni ya namna inasema kuwa katika mawasiliano kinachosemwa lazima kiwe wazi. Kusiwe na hali ya kujaribu kukisia au kujaribu kuelewa msemaji anataka kusema nini.

### **1.10 Nadharia tete**

- i) Kauli zinazotolewa na baadhi ya wahusika wajenzi katika *Mhanga Nafsi Yangu* zinakiuka kanuni ya upole.
- ii) Ukiukaji wa kanuni za upole katika *mhanga Nafsi yangu* unachochea zaidi na muktatha wa mawasiliano.
- iii) Ukiukaji wa kanuni za upole katika riwaya ya S.A. Mohammed *Mhanga Nafsi Yangu* umesaidia kuendeleza maudhui katika riwaya hiyo.
- iv) Nadharia ya upole inaweza kutumiwa kuchanganua kazi ya fasihi andishi.

### **1.11 Njia za utafiti**

Ili kuweza kufanya utafiti hii tulisoma riwaya teule ya S.A Mohammed *Mhanga Nafsi Yangu* kwa kina ili kuweza kutambua jinsi mwandishi ametumia kuishi kuboresha kazi yake. Tulisoma kazi ambazo zinzeleza kwa kina nadharia za upole ili tuwe na uelewa zaidi na hivyo kuweza kuchambua riwaya teule. Tulidurusu vitabu, tasnifu na makala yanayohusiana na utafiti wetu. Udurusu huu na usomaji wa kina tulioufanya ulituwezesha kutazama riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* katika misingi ya nadharia tuliyoichagua.

### **1.11 Hitimisho**

Katika sura hii tumeweka msingi wa utafiti ambao utatupatia mwongozo dhabiti katika utafiti wetu. Tumeeleza tulichokusudia kutafiti na madhumuni ya utafiti wetu. Pia tumeeleza sababu zilizochochea uchaguzi wa mada hii na pia tukaeleza utafiti wetu utajikita wapi. Tuliangalia yaliyoandikwa kuhusu mada kwa kuzingatia kuwa swala la upole kwa kiasi kikubwa ni la mawasiliano. Tumegusia nadharia ambayo itatuongoza katika utafiti huu na pia kuibua nadharia tete ambazo zitatuongoza. Mwisho tumeeleza njia tulizotumia katika utafiti wetu.

## SURA YA PILI

### NADHARIA YA UPOLE NA UKIUKAJI WA UPOLE KATIKA MHANGA NAFSI YANGU

#### 2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza ya tasnifu hii tumeeleza kuwa kazi hii inalenga kuangalia jinsi ukiukaji wa upole umetumiwa kujenga na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*.

Ili kuweza kufafanua mikakati ya upole katika mazungumzo, ni muhimu kuelewa nadharia za upole kikamilifu. Sura hii inafafanua nadharia mbalimbali ya upole ili kueleza jinsi upole umekiukwa katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*.

Kuna nadharia mbalimbali ambazo zimebuniwa ili kufafanua dhana ya upole. Miongoni mwa waasisi wa nadharia hizi ni Grice (1975), Lackoff (1973) Brown na Levinson (1981) na Fraser (1990)

Katika sura hii tumeangalia mitazamo minne ya Fraser (1990), mitazamo ya Brown na Levinson (1978) na mikakati ya upole ya Grice (1975). Frazer anasema kuwa dhana ya upole inaweza kushughulikiwa kwa kuzingatia mitazamo minne makuu. Mitazamo hii ni mtazamo wa mkataba wa mazungumzo, mtazamo wa kuokoa uso, mtazamo wa mazungumzo na mtazamo wa kaida za kijamii.

#### 2.1 Mitazamo ya Fraser (1990)

##### 2.1.1 Mtazamo wa upole kama mkataba wa mazungumzo

Mtazamo wa upole kama mkataba wa mazungumzo ulibuniwa na Frazer (1975) na Frazer na Nolen (1981). Mtazamo huu hutazama upole kama unaotenda kazi kulingana na mahitaji ya mkataba wa mazungumzo. Fraser (1990:232) anaeleza wakati wazungumzaji wanapoanza mazungumzo yoyote kila mshiriki wa mazungumzo huwa na uelewa wa mpangilio fulani wa haki na majukumu ambayo hubainisha jambo katika kila hatua za msingi, mambo ambayo wazungumzaji wanatarajia kutoka kwa kila mmoja wao. Hivi ni kusema kwamba msemaji na msikilizaji wana jukumu la kuhakikisha kuwa mawasiliano yanaendelezwa vizuri bila matatizo.

Kunaweza kuzuka uwezekano wa kujadili upya mkataba wa mazungumzo kwa kuwa majukumu

ya msemaji na msikilizaji yanaweza kubadilika. Mambo haya huongozwa na mazungumzo. Mikataba mingine ni ya kimsingi sana na huzingatiwa wakati mwingi watu wanapozungumza. Mikataba hii hutokana na kanuni za jumla za mazungumzo kama vile kubadilishana zamu, kutumia lugha mwafaka, kuongea kwa sauti inayosikika na nyinginezo.

### **2.1.2 Mtazamo wa mazungumzo**

Frazer (1990) anasema kuwa mtazamo wa mazungumzo hulazimishwa na asasi za kijamii zinazohusishwa na mazungumzo husika, kwa mfano wazungumzaji wanahitajika kuzungumza kwa sauti ya chini wakati wamo kanisani, matangani au maktabani. Kwenye mahakama, mshtakiwa hafai kuongea mpaka aulizwe swali. Akiongea na hajaulizwa na hakimumu kufanya hivyo huwa amevunja mkataba wa mazungumzo.

Masharti mengine katika mtazamo huu hubainika kupitia mitagusano ya awali ya washiriki. Frazer anaongeza kusema kuwa kaida hizi hutofautiana kulingana na mambo fulani fulani kama vile utambuzi wa washiriki, hadhi zao, mamlaka yao na majukumu ya kila mzungumzaji. Mambo hayo hubainisha mkondo ambao mazungumzo yatachukua. Kwa mfano, mtoto hawezi kumwamrisha mzazi wake kufanya jambo lolote na mwajiriwa hana uhuru wa kumdara mwajiri wake.

Katika mtazamo huu basi, upole unaangaliwa kama kushiriki katika mazungumzo kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa mazungumzo. Mtazamo huu hauzingatii hali ya kumfanya msikilizaji ajihisi vizuri bali unazingatia kuendeleza mazungumzo kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa mazungumzo hayo (Frazer 1990:233).

### **2.1.3 Mtazamo wa kuhifadhi uso**

Mtazamo wa kuhifadhi uso ndio uliojadiliwa zaidi ya mitazamo mingine ya kueleza dhana ya upole. Mtazamo huu ndio umetumiwa sana katika tasnifu hii ili kuchunguza ukiushi wa upole katika *Mhanga Nafsi Yangu* na jinsi ukiushi huu umetumiwa kuboresha mtindo wa riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*.

Fraser anapendekeza mtazamo huu katika kuendeleza kazi ya Brown na Levinson ya nadharia ya upole. Waasisi wa mtazamo huu ni Brown na Levinson (1978). Ili kubuni nadharia ya upole walitumia dhana ya uso ya Ervin Goffman (1967). kulingana na Goffman (1967), uso ni thamani

chanya ya kijamii ambayo mtu hujipa kulingana na mtazamo ambao wengine huchukuliana na mtazamo ambao wengine huchukulia kuwa ameegemea katika mtagusano Fulani.

Uso ni dhana bia na ni sura ya kibinafsi inayohusishwa na sifa za kijamii. Goffman (1967:9), anaendelea kusema kuwa, kutunza uso humfanya mtu kuhisi vizuri kwani tunakuwa na uhusiano wa kihisia ambao huhifadhiwa katika hali za kijamii kwa kuwa athari za kihisia za kupoteza uso zinaweza kuwa thabiti, watu mara kwa mara hushiriki katika vitendo vya kuhifadhi nyuso zao na za wengine katika mazungumzo.

Katika kuendeleza dhana ya uso, Brown na Levinson (1978) wanaeleza kuwa kuna uso chanya na uso hasi. Uso chanya ni tamanio la kutaka kukubalika na wanajamii wengine na uso hasi ni tumanio la kutaka kujiwekea mipaka ya uhuru wa kutoingiliwa. Uso chanya hutaka kutambuliwa na kuheshimiwa. Kwa mujibu wa Brown na Levinson kuna taarifa ambazo hutishia nyuso za wasikilizaji kwa sababu kuna idadi chache ya majibu yanayoweza kutolewa kuhusu taarifa hizo. Hivyo basi msemaji analazimika kuteua mikakati ya kuwasilisha taarifa ili kupunguza vitisho kwa uso wa msikilizaji. Brown na Levinson pia wanapendekeza kuwa uso unafaa kutiliwa maanani kila wakati katika mazungumzo kwa sababu unaweza kuaibishwa.

Brown na Levinson wanaongeza kuwa mikakati ya upole inayotumika katika mazungumzo inatofautiana kutegemea ni nyuso gani zinazohusika, ni nyuso chanya au nyuso hasi.

Katika *Mhanga Nafsi yangu* mwandishi ametumia baadhi ya wahusika ili kujenga na kuendeleza maudhui katika riwaya hii. Wahusika aliowatumia ni wajenzi ambao wametumia lugha inayokiuka kanuni za upole za Brown na Levinson (1987) na kanuni za upole za Frazer (1990). Nadharia hii inasema kuwa msemaji ni lazima ajiepushe kutumia maneno ambayo yanaweza kumuudhi au kumwaibisha msikilizaji. Katika riwaya hii mwandishi amewatumia wahusika wafuatao; Sheshai-za, Neshboch, Bi marneti, Bw. Bawa na Yacrobitch ili kuendeleza maudhui ya udhalilishaji na udunishaji wa wageni hasa waafrika wanapotembelea nchi za ng`ambo. Katika *Mhanga Nafsi yangu* Mhusika mkuu ni Afida na mwandishi amemtumia kuendeleza maudhui na msimamo wake kuhusu dhamira, matukio na vitushi vya hadithi yote. Mwandishi amemtumia Afida kusimamia jamii nzima ya waafrika wanapokuwa ng`ambo na masaibu wanayokumbana nayo.

Katika riwaya hii kanuni ya upole ya brown na Levinson (1978) imekiukwa kimaksudi ili



kuendeleza maudhui ya udhalilishaji. Afida anapofika Peponi anaugua kwa sababu ya baridi. Shangazi yake Bi marneti anampeleka hospitali na katika mawasiliano yake na daktari, Bi marneti anasema kuwa Afida ni mjinga na haelewi mambo ya ma-heater, anasema kuwa Afida ni mbumbumbu mzungu wa reli. Daktari naye badala ya kumshauri ajikinge kutokana na baridi kwa maneno mazuri anamwambia kuwa watu wa peponi hawafi kwa magonjwa ya ukimwi, malaria na kifua kikuu kama wafanyavyo wa Motoni. Kulingana na waasisi wa nadharia ya upole huu ni ukiushi kwa sababu maneno haya ni matusi na yanakusudia kuonyesha jinsi watu weusi walivyo nyuma. Maneno haya hata kama mwandishi hajasema chochote kuhusu hisia za Afida mawasiliano yanapoendelea ni lazima yalimuudhi Afida kwa sababu yalidhalilisha jamii yake. Kuitwa mjinga na shangazi yake pia ni jambo ambalo lingemkasirisha.

Waasisi wa nadharia hii wanapendekeza kuwa iwapo unataka kusema jambo ambalo linaweza kumuudhi au kumwaibisha msikilizaji, msemaji anafaa kutumia mkakati fulani wa upole ili aseme analotaka kusema bila kuudhi au kumwaibisha mtu. Katika mawasiliano ya Bi marneti na daktari, Bi. Marneti angeeleza kuwa ugojwa wa Afida umetokana na baridi bila kusema kuwa ni mjinga kwa sababu ametoka Motoni na hivyo haelewi mambo ya ma-heater. Daktari pia alikiuka kanuni ya Grice ya uhusiano ambayo husema kuwa mtu anafaa kusema mambo yanayohusiana na suala linalojadiliwa. Daktari alimwambia Afida kuwa watu wa Peponi hawafi kwa magojwa mabaya kama vile ukimwi, malaria na kifua kikuu. Maneno aliyoyasema hayakuwa muhimu kwa sababu magojwa yanayowauwa watu Motoni na yanayowauwa watu Peponi hayakuwa na uhusiano wowote na ugojwa wa Afida. Ukiushi huu unasaidia kuendeleza maudhui ya udhalilishaji kwa sababu mwandishi angetumia usimulizi kueleza kuwa watu weusi wanadhalilishwa bila kuwatumia wahusika hawa. Mawasiliano haya yameweka kuweka wazi hali inavyokuwa. Hata daktari ambaye kijamii anatarajiwa kuwa mpole kwa wagonjwa wake anatumia maneno ambayo yanamuudhi na kumwaibisha Afida.

Bi marneti hata kama ametoka Motoni anamdunisha Afida kwa kumwambia kuwa hata akioga mara milioni moja hawezi kuwa mweupe kama watu wa Peponi. Bi Marneti alimwambia Afida maneno hayo kwa sababu alitaka kuoga kila siku. Maneno ya Bi marneti kwa Afida yamekiuka kanuni ya upole kwa sababu angemwambia kwa upole kuwa gharama ya maji ni kubwa na wakioga kila siku malipo yatakuwa juu. Vile vile mwandishi angetumia maneno yake kueleza kuwa maji Peponi ni ghali na haikuwezekana kuoga kila siku lakini ili picha ya udunishaji

ijitokeze vizuri mwandishi aliamua kutumia ukiushi wa kanuni za upole. Kumwambia Afida kuwa hata kama akioga mara milioni moja hawezi kuwa mweupe kama wa Peponi ni kumtukana na kumwonyesha kuwa weupe ni bora kuliko weusi.

Mwandishi pia ametumia ukiushi kuendeleza maudhui ya ubaguzi wa rangi. Afida anapofika Peponi anakutana na mzee anayeitwa Neshboch na wanafunga ndoa. Dada yake Neshboch anayeitwa Sheshai-za hampendi Afida. Wakati mmoja katika mazungumzo Sheshaiza anamwambia Afida kuwa watu weusi ambao mwandishi anawaita wa-Motoni hawafai kupewa uraia wa Peponi kwa sababu Peponi ni nchi takatifu na vitakataka kama Afida hawafai kupewa uraia. Nadharia ya upole ya Brown na Levinson(1978) na Frazer (1990) kama tulivyosema awali inasema kuwa msemaji anafaa kuuhifadhi uso wa msikilizaji kwa kusema mambo ambayo hayamuudhi au kumwaibisha ili kuzuia mtafaruku. Maneno ya Sheshaiza ni matusi kwa Afida kwa sababu anaamini kuwa watu weusi hawafai kuwa sawa na watu weupe. Hata kama mtu anafaa kutumia maneno mazuri kusema jambo, katika mazungumzo haya hakuna maneno ambayo yangekubalika kwa sababu Sheshaiza hakuwa na sababu nzuri ya kusema watu weusi wasipewe uraia wa Peponi bali ni chuki na ubaguzi wa rangi uliomfanya kusema maneno haya. Kama sheshai-za angetoa kauli kuwa wa-Motoni wanapokuja Peponi kuna huduma ambazo hawapati kwa sababu yao, ingeeleweka kuwa si kuwachukia anawachukia bali ni wasiwasi kuwa maisha yao yanatatizwa na wa-Motoni.

#### **2.1.4 Mtazamo wa upole kama kaida ya kijamii**

Frazer (1990) anadai kuwa mtazamo wa upole kama kaida ya kijamii hulenga uelewa wa kihistoria wa upole ambao umekumbatiwa na watu katika jamii mbalimbali. Kila utamaduni huwa na kaida za kijamii ambazo huelekeza katika tabia fulani, hali ya mambo na namna ya kuwaza katika muktadha fulani. Upole hutokea pale ambapo kitendo kinalingana na matarajio ya jamii husika na ukiushi hutokea pale ambapo kitendo hutendeka kinyume na kaida hizo kwa mfano, katika jamii ya waafrika watoto hawataji majina ya watu wazima wanapowaita na hasa ya wazazi wao. Wanafaa kuitana mama fulani au baba fulani, shangazi, mjomba. Pia katika jamii ya Waswahili watoto ndio wanaofaa kuanza salamu kwa wakubwa kwa kuwaamkua shikamoo. Mtoto asipofanya hivyo huchukuliwa kama ukiushi wa upole.

Mtazamo huu wa upole ni jumla ya tabia nzuri na mbaya na ni dhahiri katika mazungumzo ya

jamii. Hata hivyo, kila jamii ina kaida zake ambazo zinaweza kutofautiana na za jamii nyingine. Katika jamii ya waafrika vilevile suala la mahaba halizungumziwi waziwazi na hasa mbele ya watoto. Miongoni mwa wazungu suala la mahaba ni la kawaida na linaweza kuzungumzwa na yeyote mahali popote.

Kulingana na waasisi wa nadharia hii, ukiushi hubainika pale ambapo jambo limetendeka kinyume na matarajio ya jamii. Kwa kuegemea mtazamo huu wa kijamii, mwandishi ametumia ukiushi wa upole kuendeleza maudhui ya matumaini. Ukoo\_wa Afida unapomsindikiza kwenye uwanja wa ndege, Bi Zaina bibi yake\_Afida anamwambia Afida kuwa anataka alitie bati banda lake. Afida anamuuliza kama anataka alitie bati banda lake ili amvute bwana mpya kwa sababu wanaume hutafuta paliponona na wala si sura nzuri na ujana. Bi. Zaina\_anamwambia Afida kuwa anamwonea wivu kwa sababu akitia meno atampiku kwa uzuri na ataalika ndege wazuri waje watue juu ya paa lake. Katika mawsiliano haya kuna ukiushi wa upole kwa sababu Afida na Bi. Zaina wana tofauti kubwa sana kiumri na hivyo kulingana na mila na desturi za kiafrika hawafai kuongea masuala ya mapenzi hasa mbele ya watoto. Hata kama ni mzaha, jamii haitarajii mtoto na mtu mzima kutaniana kiasi hicho. Bi Zaina angemwambia Afida anahitaji pesa za kuweka bati bila kuongeza mambo mengi ambayo si muhimu.

## **2.2 Kanuni za ushirikiano za Grice**

Kama tulivyokuwa tumesema hapo awali, Grice alipendekeza kanuni nne za ushirikiano katika mazungumzo yoyote. Kanuni hizi ni:

### **2.2.1 Kanuni ya Ubora**

Kanuni hii inasema kuwa msemaji hafai kusema jambo ambalo hawezi kulidhibitisha ukweli wake.

### **2.2.2 Kanuni ya Idadi**

Kanuni hii inasema kuwa msemaji anafaa kusema mambo ambayo yanahitajika tu. Asitumie maneno mengi ambayo hayana mchango wowote kwa yanayosemwa. Msemaji hafai kutoa habari zaidi ya zile zinazohitajika katika mazungumzo.

### **2.2.3 Kanuni ya Uhusiano**

Kanuni hii inasema kuwa msemaji ajiepushe kuingiza mambo ambayo yako nje ya mada. Hata

hivyo, wakati mwingine kanuni hii inaweza kukiukwa kwa sababu mbalimbali. Kwa mfano ikiwa mambo yanayosemwa hayamfurahishi msemaji au msikilizaji mmoja wao anaweza kubadilisha mada kimaksudi.

#### **2.2.4 Kanuni ya namna**

Kanuni hii inasema kuwa msemaji anafaa kujiepusha na kauli tata ambazo zinaweza kuibua fasiri mbalimbali. Msemaji anafaa kusema anachosema kwa uwazi.

Kanuni za ushirikiano za Grice (1975) haziwezi kufuatwa kama sheria kwani wakati mwingine msikilizaji anaweza kuwa anataka kupewa habari kwa undani kuhusu jambo fulani. Jambo kama hili linapotokea msemaji hukiuka kanuni ya idadi kimaksudi. Wakati mwingine kanuni ya namna pia inaweza kukiukwa wakati msemaji anataka kusema jambo kwa mtu mmoja na hataki wengine walielewe basi hapo anaweza kukiuka kanuni ya namna. Anaweza kusema jambo kwa njia ambayo anayelengwa ataelewa lakini waliopo ambao ujumbe si wao hawataelewa.

Ni wazi kuwa bila ushirikiano mitagusano ya watu ingekuwa jambo gumu sana na kanuni ya ushirikiano na kaida za Grice hutumika katika mitagusano ya maongezi kwa jumla. Kwa mfano, kujibu swali la maswala ya nchi kwa kueleza maswala ya nyumbani kungevunja kanuni ya uhusiano na kujibu swali la `ndio` au `la` kwa kutoa maelezo kungevunja kanuni ya idadi.

Katika *Mhanga Nafsi Yangu*, baadhi ya kanuni za ushirikiano za Grice (1975) zimekiukwa. Mwandishi amekiuka kanuni ya idadi inayosema kuwa msemaji anafaa kusema mambo yanayohitajika tu na wala asitumie maneno mengi ambayo hayana mchango wowote kwa yanayosemwa. Huu ukiushi umetumiwa kuendeleza maudhui ya matumaini. Watu wa ukoo wa Afida wana matumaini makubwa sana kuwa akienda Peponi atapata pesa nyingi na atawaletea vyote wanavyoitisha. Mwandishi amewatumia wahusika watatu ili kuendeleza maudhui haya. Amemtumia Bi. Zaina ambaye ni bibi yake Afida, mama yake Afida, shangaziye Bi. Sinango.

Katika uwanja wa ndege, Bi. Zaina anamwambia Afida kuwa angependa kwenda Peponi kutiwa meno na baada ya kutiwa meno na kurudi Motoni, apewe pesa za kutia bati. Badala ya kusema hivo moja kwa moja au mwandishi kueleza kwa kifupi, Bi Zaina anaeleza kuwa anataka aletewe tiketi aende Peponi akatiwe meno ili apate angalau jino la kutilia pozi. Anamwambia Afida kuwa anataka pesa za kutia banda lake bati ili aweze kuwaalika ndege wazuri yaani wanaume waje

kwenye nyumba yake. Kulingana na kanuni ya idadi, huu ni ukiushi na umesaidia kueleza matumaini makubwa aliyokuwa nayo Bi. Zaina.

Mwandishi pia amemtumia Bi. Sinangoa kuendeleza maudhui ya matumaini. Bi sinangoa alikuwa na shida ya tumbo ambalo lilikuwa limemsumbua kwa muda mrefu. Badala ya kumwambia Afida kuwa angependa kwenda kutibiwa Peponi, anaanza kwa kusimulia shida ambazo amekumbana nazo kutokana na ugojwa huo. Anaeleza kuwa waganga wengi wamelitibu wakashindwa, amekunya gunia zima la miti shamba na hakupona, amekunywa chupa baada ya chupa za dawa, anaeleza jinsi huchuliwa na mafuta ya uto na wachuaji wenye ujuzi na mambo mengine mengi ambayo yalimchokesha Afida. Bi Sinangoa alitumia zaidi ya nusu saa kusema jambo ambalo angesema hata kwa dakika mbili.

Katika mawasiliano haya ya Afida na Bi Sinangoa pia kuna ukiushi wa uhusiano na ubora. Kanuni ya uhusiano inasema kuwa msemaji anafaa kusema jambo ambalo lina uhusiano na mada husika. Kanuni ya ubora inasema kuwa msemaji anafaa aseme jambo ambalo anaweza kulidhibitisha ukweli wake. Bi. Sinangoa alipomaliza kueleza kadhia ya tumbo lake, alianza kuwaingilia mashehe. Anasema kuwa siku hizi hakuna mashehe na hata kama wapo, mungu hapokei dua zao. Anasema kuwa waganga wa Motoni wote ni wezi na pia madaktari hawaaminiki tena.

Bi sinangoa ameleta masuala ya mashehe na kusema kuwa siku hizi hakuna mashehe na hata kama wako hawawezi kukusemea dua ukapona. Swala la mashehe halina uhusiano wa moja kwa moja na tumbo la Bi. Sinangoa na hivyo mwandishi ametumia huo ukiushi kama njia moja ya kuonyesha matumaini makubwa aliyokuwa nayo Bi. Sinangoa kuwa atakapooenda Peponi atapata madktari wazuri watakaoweza kumtibu. Ana matumaini kuwa Afida atapata pesa nyingi ambazo zitamwezesha kulipa tiketi na kulipia gharama ya hospitali peponi.

Ukiushi wa kanuni ya ubora pia unadhihirika katika maneno ya Sinangoa kuhusu mashehe. Kanuni ya ubora inasema kuwa msemaji aseme jambo ambalo anaweza kulidhibitisha ukweli wake. Bi. Sinangoa anapoeleza shida za tumbo lake anasema kuwa motoni hakuna madaktari wala mashehe wanaoaminika na hakuna mashehe wanaoweza kukusomea dua ukapona. Hata kama Bi. Sinangoa amewahi kuombewa na mashehe akakosa kupona, ametibiwa na madaktari lakini hakupona si kweli kuwa hakuna mashehe wala madaktari wazuri.

Leech (1983) anapendekeza kanuni sita za upole ambazo ni: mkakati, ukarimu, kumsifu msikilizaji, kujitweza, makubaliano na huruma. Kwa msingi wa kaida hizi, Leech anapendekeza hali tofauti fofauti ambazo huhitaji aina tofauti za upole. Anaueleza upole kama tabia inayowaruhusu wazungumzaji kuwa katika mtagusano wa kijamii katika mazingira ya utulivu.

Hata kama kanuni za Leech (1983) zinasaidia katika mawasiliano, zinamlelea sana msemaji kwani ana jukumu la kuhakikisha kuwa ujumbe umewasilishwa bila kumuudhi au kumkasirisha msikilizaji. Hali ya kujitwetweza au kumsifu msikilizaji inaweza kumfanya msemaji kunyenyekea zaidi kwa msikilizaji. Kwa maoni yetu msikilizaji pia anafaa kuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mawasiliano yameendelezwa vizuri. Kila kaida ya Leech huandamana na kaida ndogo ambayo umuhimu wake ni mdogo. Hata hivyo kaida hizi zote huendeleza wazo kuwa upole hasi ni muhimu kuliko upole chanya. Kulingana na Leech kaida zote hazina umuhimu sawa katika mazungumzo. Kaida ya mkakati huathiri tunalosema kwa nguvu zaidi kuliko kaida ya ukarimu. Kaida ya kumsifu msikilizaji ni muhimu kuliko ile ya kujitweza. Kuna uwezekano wa kuzingatia kaida zaidi ya moja kwa wakati mmoja katika mazungumzo.

## **2.3 Kanuni za Leech (1983)**

### **2.3.1. Kaida ya mkakati**

Kaida ya mkakati inaeleza kuwa msemaji apunguze uwasilishaji wa kauli ambazo hulenga kutatiza msikilizaji na kuzidisha uwasilishaji wa kauli ambazo huwa na manufaa kwa msikilizaji. Kaida hii inalingana na mkakati hasi wa upole wa Brown na Levinson wa kupunguza ulazimishaji na mkakati chanya wa upole wa kushughulikia matamano na mahitaji ya msikilizaji.

### **2.3.2 Kaida ya kujitweza**

Kaida ya kujitweza hueleza kuwa msemaji anafaa kupunguza kauli za kujisifu au azidishe kauli za kujitweza kwa mfano "Napenda jinsi unavyopika ugali, si leo uje unipikie?" Hapa msemaji ametumia kauli ya kumsifu msikilizaji ili afanyiwe anachotaka. Pia anaweza kusema "Pilau yangu wakati mwingi huwa kama ugali, unaweza kunipikia leo?"

Hapa msemaji ametumia kauli ya kujitweza. Katika kaida hii msemaji hafai kusema lolote la kujisifu bali anafaa kumsifu msikilizaji ili apate msaada anaohitaji.

### **2.3.3 Kaida ya kumsifu msikilizaji**

Kaida hii inasema kwamba msemaji apunguze uwasilishaji wa kauli ambazo hulenga kutomsifu msikilizaji na azidishe uwasilishaji wa kauli ambazo hulenga kumsifu.

Ikiwa kwa sababu moja au nyingine msikilizaji hawezi kumsifu msikilizaji basi anafaa kutafuta njia nyingine ambazo hazitakuwa na athari chanya. Msemaji anaweza kutumia tasfida ili kuwasilisha ujumbe bila kumkasilisha msikilizaji.

### **2.3.4 Kaida ya ukarimu**

Kaida ya ukarimu inasema kuwa msemaji apunguze uwasilishaji wa kauli ambazo hulenga manufaa kwake binafsi na azidishe uwasilishaji wa kauli ambazo hulenga gharama kwake.

### **2.3.5 Kaida ya makubaliano**

Kaida hii hueleza kuwa msemaji anafaa kujiepusha na uwasilishaji wa kauli ambazo huonyesha kutokubaliana. Anafaa kuzidisha uwasilishaji wa kauli ambazo zinaonyesha makubaliano. Kaida hii ni sawa na mkakati chanya wa upole wa Levinson na Brown.

Kaida hizi zinaweza kutumiwa kama mwongozo tu kwa sababu wakati mwingine inakuwa vigumu sana kuepuka kutokubaliana. Kuna sababu nyingi sana ambazo zinaweza kuleta kutokubaliana.

### **2.3.6 Kaida ya kumwonea huruma msikilizaji**

Kaida hii hueleza kuwa msemaji apunguze kutokuwa na huruma kati yake na msikilizaji na azidishe huruma kwa msemaji. Kauli katika kaida hii ni aina ya vitendo usemi kama vile kupongeza, kutoa rambirambi, kuhimiza n.k. Msemaji anafaa kushughulikia matamaniao ya msikilizaji kwa mfano, "Nasikitika sana kwa kifo cha mamako".

Brown na Levinson walidara kanuni ya upole ya Leech na kudai kuwa ilikuwa na mikakati mingi sana. Walisema kuwa kanuni yake haikuwa na ufafanuzi toshelevu wa kaida ya kiasi, je ni kiasi kipi? Pia hakueleza kama kaida hizi ni bia au zinatumiwa katika tamaduni mahsusi pekee. Hata kama hakusema kwa maoni yetu kaida hizi huzingatiwa sana katika mawasiliano ya kawaida katika jamii. Si rahisi watu kuwasiliana katika muktatha ambao unaleta ugomvi. Jambo hili hutokea pale ambapo watu wanateta kwa sababu ya jambo Fulani.

## **2.4 Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987)**

Mtazamo wa kuhifadhi uso ndio ambao tumetumia sana katika tasnifu hii ili kuchunguza ukiushi wa upole katika riwaya ya Mhanga Nafsi Yangu na kuchunguza jinsi ukiushi huu umetumiwa kuendeleza maudhui katika riwaya hii.

Waasisi wa nadharia hii ni Brown na Levinson (1987). Ili kubuni nadharia ya Upole, walitumia dhana ya uso ya Ervin Goffman (1967).

Anasema kuwa uso ni thamani chanya ya kijamii ambayo mtu hujipa kulingana na mtazamo ambao wengine huchukuliana, na mtazamo ambao wengine huchukulia kuwa umeegemea katika mtagusano wa kijamii. Katika kuendeleza dhana ya uso, Brown na Levinson wanasema kuwa kuna uso chanya na uso hasi. Uso chanya ni tamanio la kutaka kukubalika na wanajamii wengine na uso hasi ni tamanio la kutaka kujiwekea mipaka ya uhuru wa kutoingiliwa.

Uso chanya hutaka kutambuliwa na kuheshimiwa. Brown na Levinson wanasema kuwa katika mawasiliano msemaji lazima atumie maneno ambayo hayamuudhi au kumuaibisha msikilizaji. Wanapendekeza kuwa ili kuweza kuhifadhi uso wa msikilizaji, ni lazima msemaji atumie mikakati ya upole. Wanaeleza kuwa mikakati inayotumiwa inatofautiana kutegemea ni nyuso gani zinazohusika; uso chanya au uso hasi.

Brown na Levinson (1987) wanasema kuwa kuna aina nne za vitendo vinavyotishia nyuso za wahusika katika mazungumzo. Vitendo hivi vinaweza kutishia uso wa msikilizaji au msemaji.

Aina ya kwanza ni vitendo vinavyotishia uso hasi wa msikilizaji. Vitendo hivi hutokea wakati ambapo msemaji anaingilia uso hasi wa msikilizaji kwa kuamrisha, kutoa maonyo, kushauri au hata kutoa maagizo. Kuna vitendo ambavyo hutishia uso chanya wa msikilizaji. Vitendo hivi vinaweza kumwaibisha msikilizaji na hivyo kuathiri uso chanya wake.

Vitendo vinavyoathiri uso ni kama vile kumtusi, kumtisha, kumdunisha au hata kuzungumzia mada ambazo ni mwiko katika jamii husika. Vilevile, kuna vitendo ambavyo vinatishia uso hasi wa msemaji kama vile kukubali pendekezo kutoka kwa msikilizaji, kukubali kusamehe na kuahidi kitu fulani kwa msikilizaji bila kupenda. Mwisho kuna vitendo ambavyo hutishia uso chanya wa msemaji. Vitendo hivi ni pamoja na kumwomba msikilizaji msamaha, kukubali pongezi kutoka kwa msikilizaji, kukubali makosa na kujidunisha mbele ya msikilizaji.



## **2.4. Vitendo vinavyotishia uso**

Kwa mujibu wa Levinson na Brown (1978) kuna aina nne ya vitendo vinavyotishia nyuso za wahusika katika mazungumzo. Vitendo hivi vinaweza kutishia uso wa msemaji au/na wa msikilizaji.

Aina ya kwanza ni vitendo vinavyotishia uso hasi wa msikilizaji. Vitendo hivi hutokea wakati ambapo msemaji anaingilia uso hasi wa msikilizaji kwa kuamrisha, kutoa maonyo, kushauri au hata kutoa maagizo kwa msikilizaji. Pili kuna vitendo ambavyo hutishia uso chanya wa msikilizaji. Vitendo hivi vinaweza kumtia aibu msikilizaji hivyo kuathiri uso chanya wake.

Vitendo hivi vinavyoathiri uso ni kama vile kumtusi, kumtisha, kumdunisha au hata kuzungumzia mada ambazo ni mwiko katika jamii husika. Vile vile kuna vitendo ambavyo vinatishia uso hasi wa msemaji kama vile kukubali pendekezo fulani kutoka kwa msikilizaji, kukubali kusamehe na kuahidi kitu fulani kwa msikilizaji bila kupenda. Mwisho kuna vitendo ambavyo hutishia uso chanya wa msemaji. Vitendo hivi ni pamoja na kumwomba msikilizaji msamaha, kukubali pongezi kutoka kwa msikilizaji, kukiri makosa na kujidunisha mbele ya msikilizaji.

### **2.4.1 Njia za kukabiliana na vitendo vinavyotishia**

Brown na Levinson katika nadharia yao ya upole walipendekeza mikakati mitano ya kukabiliana na vitisho kwa uso wakati wa mazungumzo. Mikakati hii ni; mkakati wa kuwa kwenye rekodi, mkakati chanya wa upole, mkakati hasi wa upole, mkakati wa nje ya rekodi na mwisho ni mkakati wa kukabiliana na vitisho kwa uso kwa kutowasilisha taarifa kabisa.

Mkakati wa kuwa kwenye rekodi hautilii maanani mahitaji yoyote ya uso. Taarifa husemwa vile ilivyo. Mkakati chanya wa upole unahusu kuonyesha heshima kwa msikilizaji na kuashiria uhusiano baina ya msemaji na msikilizaji. Mkakati hasi wa upole unapunguza ulazimishaji wa taarifa kwa msikilizaji. Mkakati wa nje ya rekodi unahusu kuwasilisha taarifa kwa njia isiyo ya moja kwa moja ambapo ni vigumu kuhusisha usemi husika moja kwa moja na hivyo kumwacha msikilizaji kufasiri usemi husika jinsi atakavyo. Huu ndio mkakati ambao msemaji hutumia methali wakati anapozungumza.

Mkakati wa mwisho ni kukabiliana na vitisho kwa uso kwa kutowasilisha ujumbe kabisa.

Mkakati huu ndio salama kabisa hata kama una kiwango kikubwa cha upole, msemaji huwa hatimizi lengo lake. Mikakati yote mitano hutumika katika mawasiliano lakini mkakati unaotumiwa hutegemea wahusika, jambo linalozungumziwa na muktatha wa mawasiliano.

Mikakati hii tumeiangalia kwa kinaganaga, tumeeleza jinsi ya kuitekeleza ili kuhifadhi nyuso za wahusika katika mazungumzo.

#### **2.4.2 Mkakati wa kuwa kwenye rekodi**

Mkakati huu hutumika wakati wazungumzaji wanafahamiana vyema. Mkakati huu kimsingi msemaji huwa hana jukumu la kuhifadhi uso wa msikilizaji. Kinachotiliwa mkazo ni ujumbe na wala sio mahitaji ya kuhifadhi uso. Mkakati huu hutumiwa katika mazingira yafuatayo.

##### **2.4.2.1 Katika hali ya dharura au kutamauka**

Mkakati huu hutumika wakati ambapo kuna hali ya dharura au kutamauka. Katika hali hii msemaji anashughulika na manufaa kwa msikilizaji wala sio kuhifadhi uso. Kwa mfano msemaji anaweza kumwambia msikilizaji "chungu, hicho kifaa kitakuangukia" au "chungu hapo mbele pana hatari." Wanaisimu wengine wameita kanuni hii kanuni' ya dharura.

##### **2.4.2.2 Katika kitendo cha kumfaidi msikilizaji**

Mkakati wa kuwa kwenye rekodi pia unatumiwa wakati tendo linalozungumziwa linamfaidi msikilizaji. Kwa mfano, msemaji anaweza kumwambia msikilizaji, "mtayarisha mtoto wako nikupelekee shule". Au "jaribu kutoka kazini mapema uje nikakununulie kinywaji" katika mawasiliano haya msikilizaji anafaidi kikamilifu na hivyo msemaji hana haja ya kuhifadhi uso wa msikilizaji.

##### **2.4.2.3 Kutoa ahadi kwa msikilizaji**

Mkakati wa kuwa kwenye rekodi pia unaweza kutumiwa wakati msikilizaji anaahidiwa kitu fulani. Katika hali hii msemaji hana haja ya kuhifadhi uso kwa sababu msikilizaji ndiye mfaidi k.m. msemaji akimwambia msikilizaji "usijisumbue kuja kwani mambo yako yote nitayaangalia vilivyo. Katika mawasiliano msemaji hana haja kuhifadhi uso wa msikilizaji kwa sababu msikilizaji ndiye mfaidi.

#### **2.4.2.4 Tofauti za kimamlaka kati ya msemaji na msikilizaji**

Mkakati wa ndani ya rekodi hutumiwa wakati msemaji na msikilizaji wako katika kiwango tofauti kimamlaka. Brown na Levinson walitambua viwango vitatu vya kisosholojia ambavyo watu huteua kiwango cha upole na pia kukadiria athari ya vitisho kwa nyuso zao. Baadhi ya vipengele hivi ni umbali kijamii na mamlaka ya wanaohusika. Mwalimu anapozungumza na mwanafunzi habitaji kutilia maanani sana kiwango cha upole lakini mwanafunzi ni lazima azingatie upole anapozungumza na mwalimu. Vile vile mwajiri na mwajiriwa, mwajiriwa atatarajiwa kuzingatia upole anapozungumza na mwajiri wake.

#### **2.5 Mkakati wa nje ya rekodi**

Mkakati huu si wa moja kwa moja. Msemaji halazimishi matamano yake kwa msikilizaji bali anadokeza tu jambo fulani na kumwacha msikilizaji afasiri ujumbe husika jinsi atakavyo. Brown na Levinson (1987:211) wanasema kuwa si rahisi kuhusisha lengo moja wazi katika usemi husika. Utata huu aidha unaafikiwa kwa kuvunja kanuni za Grice na hivyo kumwacha msikilizaji kufasiri maana ya umaanisho. Uso wa msikilizaji huhifadhiwa kwa kuwa na uwezekano wa kupata afueni katika maana halisi ya yaliyosemwa na msemaji anaweza kuuhifadhi uso wake kwa kukana kusema kauli husika. Hii ndio kanuni ambayo hutumiwa na wanasisia mara nyingi. Matumizi ya mkakati huu huwa na changamoto kwa sababu msikilizaji anaweza kufasiri ujumbe husika visivyo na hivyo kumfanya msemaji kutofanikiwa katika lengo lake. Kwa mfano, msemaji akisema "Chapati zako hunifurahisha sana".

Iwapo msemaji alitaka msikilizaji ampikie chapati anaweza kukosa kuafikia lengo lake kwa sababu si lazima msikilizaji afasiri alichotaka kusema. Msemaji anaweza kujibu kwa kusema, "watu wengi husema hivyo." Kulinganana Levinson

Brown mkakati huu ni salama kutumiwa katika juhudi za wazungumzaji lakini inamchukua msikilizaji muda mrefu kufasiri ujumbe wa msikilizaji kama anavyodhamiria. Mkakati nje ya rekodi hivyo basi huweza kutumika kwa njia zifuatazo.

##### **2.5.1 Kutumia vidokezo**

Mkakati huu huweza kutekelezwa kwa kutumia vidokezo. Msikilizaji hutoa vidokezo kuhusu jambo ambalo angetaka msikilizaji atekeleze. Kwa mfano msemaji akisema "kama ningekuwa na pesa ningenda kunywa chai" akiwa anamtaka mwenzake amnunulie chai lakini hataki

kumwambia moja kwa moja "ninunulie chai" ili kuhifadhi uso hasi wake.

### **2.5.2 Kuzua utata**

Mkakati wa nje ya rekodi pia hutumiwa kwa kuzua utata. Kuzua utata ni kusema jambo kwa njia mbalimbali. Mkakati huu unapotumiwa, msikilizaji huwa na jukumu la kutafuta fasiri inayorejelewa.

### **2.5.3 Kutumia kejeli/kinaya**

Mkakati nje ya rekodi unaweza kutumia kejeli au kinaya kama njia ya kuhifadhi nyuso za wazungumzaji. Njia hii hutumiwa wakati msemaji hataki kusema jambo moja kwa moja. Kwa mfano msemaji anaweza kumwambia msikilizaji "hapo umetumia akili kweli" wakati ambapo amefanya jambo la kijinga. Wakati mtu anapotumia mkakati huu anafaa kuwa makini anapoteua maneno kwani msikilizaji anaweza kuyafasiri maneno hayo vibaya, hivyo kutomwezesha msemaji kuafikia lengo lake.

### **2.5.4 Kutumia maswali ya balagha**

Mkakati wa nje ya rekodi hutumia maswali ya balagha. Maswali ya balagha ni maswali ambayo msemaji huwa hatarajii majibu. Mwenye kuuliza maswali ya balagha huwa ana majibu ya maswali anayouliza. Maswali haya mara nyingi hutumiwa kutilia mkazo jambo linalozungumziwa. Kwa mfano "nani asiyejua kuwa pombe haramu imemaliza vijana wetu?"

### **2.5.5 Matumizi ya sitiari**

Sitiari pia hutumiwa katika mkakati wa nje ya rekodi. Sitiari ni tamathali ya lugha ambayo neno au kirai hutumiwa kuashiria kitu kingine ambacho hakihusiani na neno au kirai hicho.

Kwa mfano, mtu anaposema "Kamau amemvunja mbuzi wa jirani mguu" katika jamii ya wakikuyu, mbuzi huashiria msichana' hivyo ni kusema Kamau amentia mimba msichana wa jirani.

## **2.6. Mkakati hasi wa upole**

Brown na Levinson (1987:129), wanaeleza kuwa mkakati hasi wa upole hutumiwa kupunguza ulazimishaji wa kauli Fulani na hautumiki kwa namna huria katika mazungumzo kama ilivyo na mkakati chanya wa upole. Mkakati huu hutumika wakati msemaji anataka kitu fulani kutoka kwa

msikilizaji lakini anataka kuhifadhi haki yake ya kukataa. Huang (2007:116), anaongeza kuwa mkakati hasi wa upole huelekea kuisitiza tofauti zilizopo baina ya msemaji na msikilizaji. Mkakati huu huchukulia kuwa msemaji atakuwa analazimisha matamano yake kwa msikilizaji hivyo basi kuna uwezekano mkubwa wa kumwaibisha kuliko mkakati chanya wa upole. Kwa lengo la kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji, msemaji anatumia mkakati hasi wa upole kwa njia zifuatazo:

### **2.6.1 Kutumia maswali na vidokezi**

Msemaji anaweza kufanikisha mkakati hasi wa upole kwa kutumia maswali na vidokezo kwa mfano, "sijui kama unaweza kunisaidia na shilingi elfu moja?" au "Unaweza kunipeleka Limuru kwa sababu matatu zimegoma?"

### **2.6.2 Kutumia vitangulizi**

Vitangulizi pia ni njia nyingine ya kupunguza vitisho vya uso katika mkakati hasi wa upole. Kitangulizi hutumiwa kama njia ya kumtayarisha msikilizaji kwa yale unayotaka kusema kwa mfano unaweza kusema "sielewi kwa nini wanawake wengine wanapenda kusifu waume zao hadharani ukisema hivi hujalenga mtu lakini ujumbe umefika na kama kunaye aliye na tabia hiyo ataelewa unavyosema na anaweza kubadilisha tabia hiyo.

### **2.6.3 Kuomba msamaha**

Msemaji anaweza kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji kwa kuomba msamaha kabla ya kutoa kauli fulani ambayo anafikiria kuwa itamfanya msikilizaji kuaibika au kuhisi vibaya. Kwa mfano "hebu nikuulize hata kama naona vigumu, Yule aliyetandikwa pale duka kuu ni kweli kuwa ni mama yako?" Au "Niwie radhi lakini nina haya ya kukwambia, tumegundua kuwa mwanao ni mwizi."

### **2.6.4 Kuonyesha heshima baina ya msemaji na msikilizaji**

Mkakati hasi wa upole pia hutumiwa kuonyesha heshima baina ya msemaji na msikilizaji ili kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji. K.m. "Mheshimiwa, najua una shughuli nyingi lakini tunakuomba uwe mgeni wetu siku ya kutuza wanafunzi." Au "Chapati zangu huwa ngumu kama mawe, si unipikie leo." Mkakati huu unalingana na kaida ya Leech ya kujitweza.

### **2.6.5 Kutaja kanuni ya jumla**

Kulingana na Levinson na Brown kutaja kanuni ya jumla ni kategoria nyingine ya mkakati hasi wa upole. Katika mkakati huu msemaji hutoa kauli inayolenga watu zaidi ya mmoja k.m. "Watu wachukue tunda moja moja ili kila mtu apate." Kauli kama hii huwa inatolewa wakati watu wanatarajiwa kujichukulia kitu na kuna mtu ama watu wanaodhaniwa kula zaidi. Ingekuwa vibaya kumwambia mtu asichukue zaidi uso kwa uso lakini kauli ya jumla ikitumiwa ujumbe hufika bila kuaibisha mtu.

### **2.6.6 Kuwa bila rajua**

Katika mkakati huu msemaji huonyesha kama ambaye hatarajii msaada kutoka kwa msikilizaji japo anauhitaji sana. Kwa mfano "sina hakika unaweza kunisaidia kwa njia yoyote lakini wacha nikwambie tu, nahitaji mahali pa kulala leo usiku." Mkakati huu hulenga kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji.

## **2.7 Mkakati chanya wa upole**

Brown na Levinson (1987:101) wanafafanua kuwa, mkakati chanya wa upole huelekezwa kwa uso chanya wa msikilizaji na tamanio lake kuwa mahitaji yake yafikiriwe kama ambayo yanatamanika. Kwa kutumia mkakati chanya wa upole, msemaji huashiria kuwa yeye na msikilizaji ni washiriki katika jambo fulani na wote wana msimamo sawa. Hivyo basi, mkakati huu hujaribu kupunguza vitisho kwa uso chanya wa msikilizaji kwa kumfanya ahisi vizuri kujihusu na kuhusu matamano yake.

Msemaji anapotumia mkakati chanya wa upole hujaribu kuwa karibu na msikilizaji kwa kuanzisha urafiki na kumheshimu kwa kumzungumzia mambo ambayo msikilizaji anapendelea na pia kujaribu kubuni mazingira yanayowatosheleza wote wawili. Mara nyingi mkakati huu hutumika katika miungano ya makundi katika jamii jambo ambalo huwafanya wanajamii kuhisi vizuri hivyo kuhifadhi na kuendeleza nyuso chanya zao. Ili kutekeleza mkakati chanya wa upole njia zifuatazo hutumika.

### **2.7.1 Kumtambua na kumshughulikia msikilizaji**

Katika mkakati chanya wa upole msemaji anamtambua msikilizaji na kumfanya ahisi vizuri. Njia hii hutumika sana katika kupongeza mtu kwa kitu kizuri alichofanya hata kama ni mavazi mazuri

aliyovaa kwa mfano "pongezi kwa matokeo mazuri, sasa utaingia chuo kikuu bila shida yoyote au "Fundu wako anaelewa kazi yake vizuri, hiyo nguo imekumpendeza sana". Kauli hizi zinahifadhi uso chanya wa msikilizaji na kumfanya ahisi vyema na kufurahi kuwa anatambulika na kukubaliwa na msemaji.

### **2.7.2 Kutumia vitambulisho vya makundi**

Msemaji pia anaweza kutumia vitambulisho vya makundi kuhifadhi uso chanya wa msikilizaji. Msikilizaji huhisi vizuri anapotambuliwa kama mwanakikundi kwa mfano, "mchango wako katika kikundi hiki umetuinua sana".

### **2.7.3 Kutafuta makubaliano**

Brown na Levinson walieleza kuwa msemaji anaweza kuhifadhi uso chanya wa msikilizaji kwa kutafuta makubaliano naye. Msemaji anaibua mada ambazo anajua kuwa msikilizaji atakubaliana nayo. Njia hii ya kutafuta makubaliano hutumika pale ambapo msemaji anaelewa msikilizaji vizuri na anajua ni mambo gani ambayo msikilizaji anakubaliana nayo na yale hakubaliani nayo.

Njia hii kwa maoni yangu huhifadhi uso wa msemaji na msikilizaji kwa sababu iwapo msemaji atatoa kauli ambayo msikilizaji hakubaliani nayo basi patatokea ubishi. Ubishi unapotokea uso chanya wa msemaji na msikilizaji vilevile huathiriwa.

### **2.7.4 Kuepuka kutokubaliana**

Njia nyingine ya kuokoa uso chanya wa msikilizaji ni kuepuka kutokubaliana au kuepuka kutopingana na msikilizaji. Kwa mfano akikuuliza kama mtaandama kwenda mahali fulani na unajua hutaweza usimwambie kuwa hutaweza bali kubali lakini umwambie atangulie mtakutana huko anakotaka mwende naye. Kauli ya kumwambia atangulie inakuruhusu kutotekeleza uliloahidi ikiwa msikilizaji ataelewa.

### **2.7.5 Kutumia ucheshi**

Msemaji pia anaweza kuokoa uso chanya wa msikilizaji kwa kutumia ucheshi. Kwa mfano msemaji anaweza kusema "Naona mwezi huu huna shughuli nyingi". Baada ya kuelezwa mambo mengi ambayo msikilizaji anafaa kutekeleza mwezi huo. Kusema hivi kutamchangamsha msikilizaji na atafanya kazi hiyo kwa furaha.

Ucheshi hutekelezwa kwa kuzungumzia mambo ya kawaida au yanayojulikana na wazungumzaji na humfanya msikilizaji kuchukulia jambo linalozungumziwa kwa wepesi.

### **2.7.6 Kuwa mrijua**

Msemaji anapotumia njia ya kuwa mrijua huwa na mwelekeo chanya kuwa msikilizaji atatekeleza agizo ambalo atamwagiza. Kwa mfano "Utanoshea nyumba leo, sivyo?" au "kesho asubuhi ni wewe utakamua ngombe, sivyo?"

Kwa kudhihirisha urijua, msemaji anamshawishi msikilizaji kutekeleza agizo husika ili azidi kukubalika na msemaji. Mkakati huu hutumika wakati wahusika wana uhusiano wa kimamlaka na msemaji ana mamlaka juu ya msikilizaji. Kwa mfano, mzazi na mtoto, mwajiri na mwajiriwa miongoni mwa mahusiano mengine ya kimamlaka katika jamii.

### **2.7.7 Kuuliza au kutoa sababu za kitendo fulani**

Upole chanya pia unaweza kutekelezwa kwa kuuliza au kutoa sababu za kutenda kitendo fulani kwa mfano, "Kwa nini usifue sasa ili nguo zikauke kabla jua halijatua?." Unapotumia mkakati huu huwa unaepuka kumwamrisha msikilizaji na hivyo kuhifadhi uso wake.

### **2.7.8 Mkakati wa kutotekeleza kitendo kinachotishia uso**

Kando na mikakati minne ya kukabiliana na vitendo vinavyotishia nyuso za wazungumzaji iliyojadiliwa, Brown na Levinson pia walipendekeza mkakati wa tano ambao ni kutosema ujumbe unaofikiriwa kuwa tishio kwa uso wa msikilizaji. Mkakati huu ndio salama zaidi kuliko mikakati mingine lakini una hatari kwamba msemaji akiamua kuutumia hauafikii lengo lake. Kwa mfano, ikiwa msemaji alikuwa anataka afanyiwe au apewe kitu fulani, na afanye uamuzi wa kutoomba kufanyiwa au kupewa kitu hicho basi hitaji lake litabakia pale pale. Katika mikakati mingine, analotaka msemaji litaafikiwa hata kama njia au mkakati utakaotumiwa kuomba jambo ni tofauti.

Katika *Mhanga Nafsi Yangu* mwandishi ametumia ukiushi wa nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1978) kuendeleza maudhui ya dhuluma, maonevu na udunishaji wa watu weusi. Nadharia ya upole ya Brown na Levinson inasema kuwa kuna uso chanya na uso hasi na nyuso zote mbili hutaka kuhifadhiwa katika mawasiliano. Msemaji anafaa kujiepusha na kutumia maneno au kauli zinazoweza kumwaibisha au kumuudhi msikilizaji. Vitendo hivi ni kama



kumtusi mtu, kumtisha, kumdunisha au kuzungumzia mada ambazo ni mwiko katika jamii husika.

Afida anapofika Peponi anaenda kuishi na Shangazi yake Bi. Marneti ambaye ndiye aliyemwalika. Baada ya muda mfupi, Bi. Marneti anaanza kumshuku mumewe kuwa anampenda Afida. Bi. Marneti anapompeleka Afida zahanatini baada ya Afida kuugua homa kali, anamwonya dhidi ya kuyatazama macho ya mwani ya mumewe. Afida anashangaa ni vipi shangazi yake anaweza kumwambia maneno kama yale. Kulingana na Afida, mwanya wa marika kati yake na Bi. Marneti hauruhusu wao kujadiliana jambo kama hilo. Afida anasema; "hata ingekuwaje, kule kwetu Motoni, mtu angeshangazwa kwa mwanya wa marika ulio wazi baina ya mimi na yeye." Ukiushi huu ambao umejikita katika misingi ya kijamii unaonyesha jinsi Afida anavyokumbana na maonevu hata na shangazi yake ambaye anatarajia amsaidie mpaka azoe maisha ya ugenini. Kawaida mtu anafaa kuzingatia umri wa anayezungumza naye ili kuepuka kumuudhi au kumwaibisha msikilizaji. Kama tunavyoona, baada ya Afida kuambiwa maneno haya alianza kulia kuonyesha kuwa uso hasi wake haukuhifidhiwa. Kama Bi. Marneti alitaka kumpa Afida nasaha angemketisha chini kama mzazi badala ya kumwingilia kama mama wa rika lake.

Mwandishi pia amemtumia Bw. Bawa kuendeleza maudhui ya udunishaji wa watu weusi wakiwa Peponi. Hata kama amemwoa Bi. Marneti bado anamchukulia kama m-Motoni tu. Wivu wa Bi. Marneti unaleta ugomvi nyumbani kwao na Bi. Marneti anasisitiza kuwa lazima Afida atoke pale. Katika mtafaruku huo, Bw. Bawa anamwambia Bi Marneti kuwa wanaume wa Peponi na hata wanawake hawapendi wivu wa kipumbavu kama alionao mkewe. Anamuuliza ana kipimo gani au uchawi gani kujua kuwa yeye na Afida wanatazamana kimapenzi, na mwishowe anamwambia aache wivu wa kitoto. Bi. Marneti anamwambia mumewe kuwa lazima Afida aende shule. Mumewe anamuuliza kama amelifikiria suala la pesa. Swali hili linamuudhi na anamwambia mumewe kuwa yeye kila kitu lazima aseme hakuna pesa. Ugomvi huu unafikia kilele wakati Bw. Bawa anamwambia mkewe kuwa kwao Motoni hakuna kitu kinachoendelea isipokuwa umaskini, maradhi na ombaomba.

Katika mazungumzo hayo Bw. Bawa anamtukana mkewe kwa kumkumbusha kuwa yeye ni m-Motoni na huko Motoni hakuna jambo nzuri linalopatikana huko. Bw. Bawa hajali kumkasirisha mkewe na hivyo hauhifadhi uso hasi wa Bi. Marneti. Kwa kuwa huyu ni mtu na mkewe

wangekaa wazungumze bila kutumia matusi. Kulingana na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987), matusi hayafai kutumiwa katika mawasiliano na yanapotumiwa huwa ukiushi wa upole. Kwa kutumia ukiushi huu mwandishi amefaulu kuonyesha jinsi watu weusi wanavyochukuliwa wakiwa nchi za ng`ambo.

Mwandishi pia ametumia ukiushi kwa kutumia Neshboch ambaye alikuwa mumewe Afida. Bi. Marneti anapanga kuwa Afida aolewe na Neshboch lakini akipata mtoto ampatie Bi. Marneti kwa sababu hana mtoto. Baada ya Afida kupata mtoto anakataa kumpeana. Maisha ya ndoa kati yake na Neshboch yanazidi kuzorota na Afida anafukuzwa.

Baada ya muda Afida anarudi lakini hali haijabadilika sana. Siku moja Afida anampelekea mumewe chakula na badala ya kukipokea anamtukana Afida. Anamwambia kuwa yeye hataki kula chakula kichafu na kisicho thamani. Afida anapomkumbusha jinsi alivyokuwa akiramba sahani kwa vidole na ulimi anamwambia kuwa hakukuwa kuramba mbali kulikuwa kusafisha takataka za sahani tu. Neshboch anamwambia Afida kuwa ana bahati kuolewa naye kwa sababu wa Motoni hawastahiki kuolewa na wa Peponi kwa sababu walikuwa watumwa wao.

Kulingana na nadharia ya upole, mawasiliano yanafaa kuendelezwa kwa njia nzuri ambayo msemaji na msikilizaji wanaelewana. Uso hasi wa msemaji na msikilizaji unafaa kuhifadhiwa. Hakuna anayefaa kuudhi mwingine na hili linapotokea kama katika mawasiliano ya Afida na Neshboch basi huwa upole umekiukwa. Katika mawasiliano ya Neshboch na Afida, walikuwa wanajibishana hata kama alikuwa anajibu baada ya kutukanwa na mumewe. Neshboch anapomwambia Afida kuwa alimwokota njiani, Afida anamwambia kuwa hana akili ikiwa anaweza kuzoa na kutia takataka na uchafu nyumbani kwake.

Ukiushi huu umeendeleza maudhui ya maonevu na udhalilishaji kwa sababu mwandishi angetumia maelezo kuonyesha jinsi Neshboch anavyowadharau watu weusi. Neshboch ametumiwa vizuri kusimamia watu wa nchi za ng`ambo kuonyesha wanavyowadharau watu weusi.

*Katika Mhanga Nafsi Yangu*, Afida amekuwa kama chombo cha watu wa Peponi, kutukanwa na hata kudhulumiwa. Anapokonywa mtoto wake kwa kisingizio kuwa yeye ni mlevi na hata hawezi kulea mtoto. Afida anapoambiwa na Bi. Marneti kuwa anamnyemelea mumewe hasemi chochote bali ananyamaza na kulia tu. Rafiki yake shuhuda anapomwambia atumie mwili wake

kama mwanamke anaudhika lakini hamjibu. Baadaye tunamwona Afida akibadilika na anapotukanwa na Neshboch anamjibu kwa matusi pia. Afida anapopokonywa mtoto anakuwa mlevi kupindukia na hata anaingilia ukahaba. Siku moja akiwa kwenye baa anaropokwa maneno ambayo hayafai kusemwa mbele ya watu kwa sababu ni maneno ya aibu. Anasema kwa sauti kuwa anataka kutiwa mimba kwa sababu alipokonywa mtoto wake. Kawaida mtu mwenye akili timamu hawezi kuropokwa maneno kama hayo.

Hii inaonyesha kuwa ukiushi wa upole unaweza kuchochewa na muktatha wa mawasiliano na jambo linalojadiliwa. Hisia za msemaji na msikilizaji pia zinaweza kuchochea ukiushi wa kanuni ya upole kwa sababu mtu anapokasirika anashindwa kujizuia na anaweza kutumia lugha ya matusi kama tunavyomwona Afida akifanya.

## **2.8 Hitimisho**

Katika sura hii tumeangazia nadharia zilizobuniwa ili kueleza dhana ya upole katika mitagusano ya kijamii.

Tumeangalia nadharia ya ushirikiano ya Grice, Kanuni za upole za Lackoff na Leech, na nadharia ya uso ya Brown na Levinson, zote hizi ni namna za kufafanua dhana ya upole na jinsi upole hushughulikiwa katika mazungumzo ya kila siku. Tungepata kutaja hapa kuwa kakuna nadharia bora kuliko nyingine ila misingi ya nadharia hizi hutofautisha miktadha ambamo nadharia hizi hutumika katika mahusiano ya kila siku.

Katika nadharia ya uso mikakati iliyojadiliwa ilipendekezwa na Brown na Levinson. Inazungumzia jinsi ya kukabiliana na vitendo vinavyotishia nyuso za wahusika katika mazungumzo mbalimbali. Waasisi wa nadharia hii walieleza kuwa masuala yanayohusu uso ni tofauti katika tamaduni mbalimbali japo dhana za uso hasi na uso chanya zinapatikana katika tamaduni zote ulimwenguni. Katika tasnifu hii tumejikita kwa kanuni za ushirikiano za Grice na nadharia ya upole ya Brown na Levinson. Tumetumia nadharia hizi kuonyesha jinsi S.A. Mohamed ametumia ukiushi wa kanuni za upole kujenga na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*. Tumeonyesha jinsi ametumia baadhi ya wahusika kuendeleza dhamira kuu katika *Mhanga Nafsi Yangu*.

## SURA YA TATU

### MATUMIZI YA LUGHA KATIKA *MHANGA NAFSI YANGU*

#### 3.0. Utangulizi

Kimani na Chimerah (1999) kwa mujibu wa mhakiki wa kirusi Roman Jacobson, "fasihi ni matumizi ya nguvu dhidi ya nguvu ya kawaida kimakusudi." Katika kauli hii Jacobson ana maana kuwa fasihi huichukua lugha ya kawaida halafu anaifinyanga, anaiunda huku na huku hadi akaifanya ipendeze. Hivi ni kusema kwamba, kile kinachosemwa kifasihi huwa kimeinuliwa kwa matumizi ya lugha hivi kwamba mdundo wake si wa kawaida. Hivyo, fasihi ni matumizi ya lugha kwa ufasaha.

Kirumbi (1975) anasema kuwa, "tusemapo kuwa fasihi inajengwa kwa maneno na lazima maneno hayo yawe ni maneno zaidi ya maneno mengine, fasihi si kuwa na maneno ya kisanaa, bali ni kutumia maneno ya kila siku kisanaa.

Wamitila (2003) anakubaliana na kauli ya Kirumbi na kuisitiza kuwa lugha ndiyo nyenzo inayotofautisha fasihi na sanaa nyingine kama vile uchoraji, ususi, ufinyanzi na nyinginezo.

Katika sura hii tutaangalia mbinu mbalimbali ambazo S.A. Mohamed ametumia kujenga maudhui katika *Mhanga Nafsi Yangu*. Tutaangalia jinsi mwandishi ametumia lugha kuendeleza maudhui katika *Mhanga Nafsi Yangu*. Tutaangalia matumizi ya methali, misemo, mbinu rejeshi, uzungumzi nafsi, nyimbo, tanakali za sauti, urudiaji, kuchanganya ndimi, tashbihi na ukiukaji wa kanuni za upole.

Kwa kuwa mojawapo wa madhumuni ya kazi hii ni kuchunguza jinsi mwandishi alivyotumia ukiushi kuendeleza maudhui, tutaangalia ukiushi wa kanuni za upole kama mbinu inayotumiwa kuendeleza maudhui katika riwaya hii.

#### 3.1 Mbinu zilizotumiwa kujenga na kuendeleza maudhui katika *Mhanga Nafsi Yangu*.

##### 3.1.1 Uzungumzi Nafsi

Wamitila (2003) alieleza kuwa uzungumzi nafisia huelezea maongezi au hotuba ndefu inayotolewa na mhusika mmoja ili kukuza tendo kuu la hadithi. Mbinu hii hutumiwa na mwandishi kuwafunulia watazamaji au wasomaji mawazo ya mhusika. Hii mbinu husaidia kuelewa hisia za mhusika. Mbinu hii imetumiwa na mwandishi kuendeleza maudhui ya huzuni

na majuto aliyokuwa nayo mhusika mkuu alipokuwa Peponi. Mara kwa mara Afida alikuwa akijizungumzia mwenyewe alipokumbuka nyumbani. Mbinu hii imetumiwa kuendeleza maudhui ya kutegemeana. Afida anashangaa jinsi waafrika wanavyokaa na kutegemea msaada kutoka kwa wanaofanikiwa. Afida analalamika kuwa watu hata hawangojei mtu afanikiwe ili waanze kudai hiki na kile bali wanaanza kuitisha hata kabla mafanikio hayo hayajaonekana. Mawazo haya ya Afida yanachochewa na matukio katika uwanja wa ndege wakati watu wa ukoo wake walipomsindikiza. Kila mtu alikuwa na mlolongo wa mahitaji ambayo walitarajia Afida atimize afikapo Peponi.

".....Sisi waafrika lazima tugawane mafanikio hata kabla mafanikio hayajazaliwa.....Aliyefanikiwa ni mateka anayeangushwa na kunyofolewa nyama haraka haraka na kumegwa kila upande mpaka anapobakishwa mifupa mitupu."uk. 6

Afida anazidi kueleza kuwa watu wa ukoo hufanya hivyo eti kwa sababu pia wao walimsaidia mtu alipokuwa mdogo. Mawazo ya Afida yanaeleza jinsi mambo yalivyo hata katika hali halisi ya maisha. Mtu anaposoma na kupata kazi na hasa akipata kazi nchi za ng'ambo kila mtu aliyekusaidia anatarajia utamlipa kwa njia moja au nyingine. Hata wale ambao hawakuhusika katika malezi yako hutaka pia kupewa.

Baada ya kuishi Peponi kwa miaka mingi na maisha kumwendea mrama Afida anaanza kujuta kwa maisha anayoishi. Anaanza kujiuliza maswali ambayo hawezi kuyajibu. Katika kujizungumzia kwa Afida tunaona anavyojuta kwa kujiharibia maisha. Afida anaongea na nafsi yake kama ambaye anaongea na mtu mwingine:

".....Kwa nini fikra ya ulevi imemganda kichwani haitaki kumtoka. Kwanini hataki kufikiri.....Kwanini kajiachia namna hii kiasi cha kuchukua upande mbaya wa uhuru wake? Uhuru wa kuuza ovyo mwili wake? Kuuza kwa chupa moja tu ya bia....."  
uk. 179

### **3.1.2. Nyimbo**

Nyimbo zimetumiwa kuendeleza maudhui ya utamaduni. Afida anakumbuka jinsi huko motoni

watu walivyokuwa wakiimba kumfurahisha muumba. Anakumbuka jinsi nyimbo zilizoimbwa zilivyoakisi maisha ya kila siku ya motoni. Afida anaeleza ngoma mbalimbali na miondoko mbalimbali iliyomvutia huko motoni. Anakumbuka wimbo mmoja uliowatia wazee na wazazi wasiwasi hata kama hajaeleza wasiwasi ulikuwa wa nini. "Bonge lote hilo umenipa kidogo mkononi kuonja." Uk. 129

Afida pia alikumbuka jinsi mama yao alivyowahadithia hadithi zilizoeleza jinsi mwanamke anayeolewa anavyohisi kicwani juu ya mwanawe na ndoa yake. Katika tamaduni za waafrika, mwanamke alitarajiwa kuvumilia maisha ya ndoa hata yakiwa magumu. Alitatajiwa kuwatunza watoto wake na kuwatuliza hata kama yeye hana wa kumtuliza. Anakumbuka wimbo aliowaimbia mama yao kila walipolia;

"Howa howa mtoto siliye mwana siliye  
ukaniliza na miye machozi yako yaweke  
nikifa unililiye upigepige mateke watu  
wakushikilie...." Uk 159

Wimbo huu umerudiwa tena na mara hii unaimbwa na Afida na Sapataro wanapotoka ulevini. Katika wimbo wa pili wa Afida na Sapataro, unachochea na ulevi na wala hauashirii utamaduni wowote. Katika mila na desturi za waafrika ngano na nyimbo zilikua kama jambo la lazima. Jioni baada ya kazi watoto waliketi na wazee na kuhadithiwa hadithi zenye mafunzo. Utamaduni huu ndio Afida anakumbuka akiwa peponi. Mbinu hii ikiwa ya fasihi simulizi, inaonyesha jinsi fasihi simulizi inaendelea kuirutubisha fasihi andishi hasa ya kiafrika.

### **3.1.3 Misemo**

Misemo ni matumizi ya lugha ya kawaida kijozi kwa njia isiyokuwa ya kawaida. Misemo huhitaji mtu afikirie sana kwanza ndiposa afichue maana ya maneno husika.

Mwandishi ametumia mbinu hii katika riwaya hii. Afida alipohama na kwenda kuishi peke yake, wakati mwingi mawazo yalimtatiza kwa shida alizopata nyumbani kwa Bi Marneti. Katika hali yake ya kuwaza na kuwazua, anasema kuwa hataki kukaa na watu wenye damu, nyama na mifupa kama yeye. Yeye anaona kuwa watu wote ni wanafiki na hivyo anataka kujisemea mwenyewe. Afida anasema kuwa hataki kusema na mtu anayempaka mafuta nyuma ya mgongo wa chupa.

Afida ana machungu kwa sababu shangazi yake anasingizia kuwa anamnyemelea mume wake. Anampeleka chuo ili aondoke pale nyumbani lakini anajifanya kuwa anataka Afida apate elimu. Kupaka mtu mafuta kwa mgongo wa chupa ni kujifanya kuwa unampenda mtu na ndani ya moyo wako unamchukia.

Afida akiwaza kuhusu Bi Marneti na anavyomdhanika, anashangaa ni vipi shangazie anaweza kumfikiria kuwa anaweza kuwa na na uhusiano na mumewe ambaye amekomaa sana kilinganishwa na Afida.

"... kwa nini niende na huyu babu anayeitwa Bawa? Mungu ataninusuru! Naelewa kwamba wanaume hata wanaporegea kama mboga na kupoteza nguvu zao za radi... Yaani wanajidai kuwa ndiyo kwanza mkoko ualike maua" uk. 88

Katika maneno hayo mwandishi ametumia semi anapoongea kuhusu "mwanaume kuregea kama mboga" kwa maana kuwa mwanamume amezeeka na kisha anasema kuwa "wanajidai ndiyo kwanza mkoko ualike maua" yaani wanajidai kuwa bado ni vijana.

Katika aya ya pili ya ukurasa huo mwandishi ametumia semi. Afida anazidi kueleza uchungu wake na mwishowe anasema :

"Anayeongozwa na mshawasha hawachi kuchonotwa na fikira mbovu na hasa anapodhani kuwa kitumbua chake kinatiwa mchanga!" uk 89

Huyu anayeongozwa na fikira mbaya, ni Bi Marneti na hicho kitumbua kinachotiwa mchanga ni mapenzi yake Bi Marneti na Bw Bawa. Bi Marneti siku zote amekuwa akidhani kuwa Afida atamchukua mumewe. Anasema kuwa Bi Marneti anaona kama siku moja 'atamtia mumewe mkobani'

Baada ya Afida kuonywa kuwa angerejeshwa motoni alishikwa na maradhi ambayo yalimwadhiri mwili. Bi Marneti kwa kuwa aliona Afida ameshituka alipoambiwa angerudishwa motoni aliamua kutumia nafasi hiyo kumuondoa nyumbani kwake kabisa. Mwandishi anasema kuwa Bi Marneti "alipiga ndege wawili kwa jiwe moja" Kwa kusema hivyo alimaanisha Bi Marneti alijiondolea shida ya kumuuguzwa Afida na pia akajiondolea usumbufu wa kumlinda

mumewe asichukuliwe na Afida.

#### **3.1.4. Methali**

Mwandishi pia ametumia methali ili kuendeleza maudhui katika *Mhanga Nafsi Yangu*. Afida anapoanza kufikiria watu aliowaacha motoni na hasa Shabaan, anasema kuwa kumsahau kwake shabaan na mapenzi yao na hata ahadi ya ndoa kunaweza kumithilishwa na methali isemayo "asiyekuwapo na lake halipo"

Mwandishi pia ametumia methali kuonyesha ujanja wa Afida alipokuwa akiburudika na Saparato. Afida kabla ya kuharibiwa na maisha ya peponi alikuwa msichana mzuri na mwenye tabia nzuri. Alipokutana na Saparato na Saparato akawa anataka kumwingiza kwenye mtego wa mapenzi, Afida siku zote alicheka hata kama aliyoyasema Saparato hayakumfurahisha. Alisema kuwa alikuwa anacheza mchezo wake kiungwana kwani waswahili hunena, "Muungwana hanuni mashavu" Kwa sababu ya hii tabia Saparato hakuweza kumwelewa Afida na hivyo hakufanikiwa kumdhulumu kimapenzi kama alivyo zoea kuwafanya wasichana wengine.

Afida anapoeleza kuhusu ushuba wao na Neshboch anasema kuwa baada ya kukaa na Neshboch walikuwa wamezoeana na hivyo alipomwomba waende nyumbani kwake wakale chakula inaonyesha kuwa alikuwa ameombwa siku nyingine na kukataa lakini mara hii anakubali, anasema: "si unajua tena watu husema papo kwa hapo kamba hukata jiwe." Uk. 40

#### **3.1.5. Tanakali za sauti**

Tanakali za sauti pia zimetumika katika riwaya hii. Tanakali za sauti ni njia moja inayotumiwa kuonyesha au kueleza jinsi jambo lilivyofanyika. Wakati Afida anapopelekwa hospitali na Bi Marnetti alianza kumuonya Afida dhidi ya kumwangukia mumewe kwa macho ya mwani. Afida alihisi uchungu moyoni na ndipo akaanza kulia. Afida katika kueleza uchungu wake anasema:

"Hilo sasa likazidi kuchimbua kilio changu.  
Kikajitokeza waziwazi kwa kekefu na kwi  
kwi. Mradi machozi kupukupu, kamasi  
frufu...." Uk 36

Maneno haya au tanakali hizi za sauti kuonyesha alivyolia Afida zinasaidia kuonyesha uchungu na huzuni uliomkumba Afida.

Mwandishi kwa kueleza ukali wa baridi ya peponi anaeleza jinsi huwa wanajifunika gubigubi



wakati wa baridi. Afida anapojaribu kumweleza mzee Bawa kuhusu uekevu wa fasihi ndani ya maisha ya jamii, Bw. Bawa alikataa katakata aliyosema Afida. "Katakata" inasisitiza jinsi Bw. Bawa alivyopinga kauli ya Afida kuhusu Peponi. Tanakali hiyo pia imetumiwa kuonyesha jinsi Afida alivyokataa maneno ya Yakrobich pale ambapo anamfuata ili wacheze "mchezo wa kufurahisha mwili". Afida anasema kuwa alikataa kabisa kushiriki ngono kwa sababu yeye hakuamini kuwa kushiriki ngono ilikuwa jambo la kufurahisha.

### **3.1.6. Tashbihi**

Tashbihi ni mbinu ambayo mwandishi analinganisha kitu na kingine au jambo na jingine kwa kutumia maneno kama mithili ya, ja na kama katika ulinganifu huo. Tashbihi imetumiwa kuonyesha jinsi baridi ya peponi ilivyomwingia Afida. Anaeleza jinsi alivyotoka nyumbani wakati wa baridi na alipokuwa kwenye stani alikuwa anatemeka. Anatumia tashbihi ili kuonyesha jinsi baridi ilivyokuwa kali;

"Nilipojipeleleza tena nilijikuta ninatemeka kama ukuti Wa mnazi ulioingia pepo. Wakati kama huu nilikuwa naogopa sana kungojea basi." Uk 57

"Lakini wapi, baridi haikutaka kusikia. Alijikuta tu Afida baridi inampenya mpaka ndani ya mifupa yake, mpaka ikamfanya ang`ang`anae kama samaki aliyeganda kwenye freezer." Uk 30

Afida vilevile kwa kueleza ukubwa wa mananasi ya Motoni anasema kuwa mananasi ya Peponi kila siku ni makubwa kama kichwa cha ng`ombe. Shuhuda alipokuwa akieleza kufanana kwake na Afida anasema kuwa wanafanana kama sahani na kawa. Afida anamweleza shuhuda kama msichana mrembo lakini anakerwa na tabia yake ya uvutaji sigara. Anasema kuwa yeye na shuhuda hukosana kwa sababu ya tabia hiyo lakini Shuhuda hasikii. Afida anamweleza Shuhuda kama msichana mkaidi kama mkia wa punda. Hii tashbihi imetumika kuonyesha kiwango cha ukaidi wa shuhuda. Tashbihi pia imetumika kuonyesha jinsi Saparato alivyojaribu kumpata Afida. Saparato alijaribu kumfuata Afida kwa kumwekea mtego. Anaeleza kuwa Saparato alikuwa akimwangalia kwa macho yaliyokuwa yanaonyewa wazi alivyomtamani Afida;

"Mboni zake zinazowaka buluu hazikutulizana. Zilipanda juu na kushuka

chini harakaharaka kama dira inayokagua  
kiwiliwili changu waziwazi nje na kisirisiri  
ndani." Uk. 82

Baada ya muda mrefu baada ya Afida kupata mtoto wa Sapataro walikutana tena kwa Sadfa tu. Afida alikuwa na mtoto wake waliozaa na Sapataro. Sapataro alipomuona mtoto alisema kuwa walifanana na Afida kama reale kwa ya pili. Alisema kuwa mtoto alimranda tu pua. Maneno haya yalikuwa ya kumdhalilisha Afida kwa sababu baada ya kuzungumza kwa muda mfupi alimwambia Afida kuwa huyo mtoto hangekubaliwa na wazazi wake kwa sababu hakufanana na mtu yeyote wa ukoo wao.

### **3.1.7. Kuchanganya Ndimi**

Kuchanganya ndimi ni kutumia lugha tofauti na ile iliyotumiwa katika kazi nzima ya fasihi. Mara nyingi hii mbinu hutumiwa wakati kuna jambo ambalo mwandishi anataka kuisisitiza. Katika hali halisia watu huchanganya ndimi kwa sababu tofauti tofauti. Mbinu hii imetumiwa pale ambapo Afida anapanda ndege kwenda Peponi. Afida anapopanda ndege, anashtukia ameguswa kwa mkono begani na anapoangalia hamwoni mtu yeyote. Babake Afida alikuwa akimtokea mara kwa mara na wakati huu alikuwa amekuja kumpa nasaha. Baada ya Afida kusikiliza kama ambaye alikuwa anamuona baba yake anajibu kwa kusema "Nimesikia." Jirani yake kwenye ndege anafikiria anaongea nayeye. Anamjibu Afida kwa kusema "sorry" kwa maana kuwa hakisikia alichosema Afida. Afida anamwambia jirani yake kwamba hakuwa amesema kitu lakini huyo mtu alisisitiza;

*"But you are muttering something and  
shading tears... Is it your first time to  
travel? Are you missing your  
people....Where exactly are you heading  
to?" uk. 15*

Mwandishi kwa kueleza jinsi watu wa nchi mbalimbali wanavyochukuliwa anaeleza kuwa kuna *'the developed World', 'the civilized world', 'first developing world au underdeveloped world.'* Maneno haya yametumiwa na Afida ili kuonyesha jinsi watu huheshimiwa duniani kulingana na walivyoendelea hasa kiuchumi na kiteknolojia.

Katika kueleza mambo yalivyo duniani, mwandishi amemtumia Afida akizungumza na kivuli cha marehemu baba yake. Anamwambia baba yake jinsi dunia ilivyo.

".... hapa hapana imani tena, pana kunyonya damu tu kama enzi za Dracula anayetongoza watu kwa kauli ya *you are my darling!*" uk 95

Kuhusu vitu, sijui kama umewahi kumsikia DBC Piere anavyosema: *Look at it my friend: all has ever been called love of life, is love of things that won't happen.....*"

Mbinu hii pia imetumika wakati Afida anazua vurugu kwenye klabu. Mwenye klabu kwa ghathabu anamwambia Afida; "Sharraap!" naye Afida anamjibu kwa hasira; "damn it, am not going to sharraap." Afida alikuwa anaonyesha uchungu wake anapokumbuka kuwa alipokonywa mtoto. Mwandishi pia ametumia lugha ya kiarabu. Afida anaeleza jinsi walivyokuwa wakifunzwa kusoma huko Motoni.

"Abjad alif bee jim dal.....alif, bee, tee, thee" uk. 111

Kuna maneno mengine ambayo yametumiwa kueleza dhana mbalimbali kama vile *morality, human happiness, mechanism of desire* na mengine mengi.

### **3.1.8. Urudiaji**

Mwandishi pia ametumia urudiaji. Hii ni mbinu ambayo neno au kikundi cha maneno hurudiwarudiwa. Uradidi huwa ni njia moja ya kusisitiza jambo. Mwandishi ametumia uradidi katika mawasiliano ya Bw Bawa na Bi Marneti. Mawasiliano hayo ni ya ugomvi.

"....Aaa tuyaaache hayo marumbano ya kila siku yasiyokwisha."

"....kuna sababu lakini ya kujirudiarudia. Na yakiwa yanajirudiarudia hatuna budi kuyazingatia" uk. 42

Maneno haya yanaonyesha kuwa kuwepo kwa Afida nyumbani kwa shangaziye kulikuwa kunaleta ugomvi kwa mtu na mumewe. Mwandishi ametumia uradidi kueleza hali ilivyokuwa katika nyumba ya Bi Marneti. Amemtumia Afida kueleza aliyokumbana nayo pale nyumbani. Afida anaeleza kuwa hata kama watu hawatoki jumapili yeye aliamua kutoroka kelele za pale nyumbani.

".... juu ya hiyo ilinibidi kutoka ndani kukimbia kusema kweli. Nilihisi bora baridi ya nje kuliko ujotojoto wa ndani. Bora

zururazurura ya nje, kwa hivyo nilitoka nje  
nikiichangamkia fikra ya kujikinga na baridi  
kwa manguo niliyojizongazonga nayo  
mwilini" uk. 58

Ujotojoto ambao Afida anaouzungumzia ni kelele za mara kwa mara za Bi Marneti. Pia anaeleza baridi kali iliyokuwa nje kwa kueleza alivyovaa alipotoka.

### **3.1.9 Mbinu Rejeshi**

Mwandishi pia ametumia mbinu rejeshi katika riwaya hii. Mbinu rejeshi ni hali ya kurudi nyuma kuyakumbuka mambo ambayo yalikuwa yametendeka awali. Ameitumia mbinu hii kuonyesha matumaini ya ukoo wa Afida. Anaeleza jinsi mambo yalivyokuwa katika uwanja wa ndege. Kila mtu alikuwa na matumaini kuwa Afida angebarikiwa na kuwaletea vitu walivyoagiza. Kwa kutumia mbinu hii mwandishi ameweka wazi jinsi mambo huwa katika hali halisia. Mtu anaposafiri kwenda nchi za mbali, kila mtu huwa na matumaini kuwa anayeenda atatajirika na kuwatoa kwenye umaskini wao.

Mbinu hii pia imetumika kueleza jinsi ubaridi wa peponi unavyomnyima Afida usingizi. Anasema kuwa kukosa usingizi halikuwa jambo geni kwake kwani alipokuwa mdogo alikuwa anashindwa kulala baada ya kusikiliza hadithi za viumbe katili, maharamia na mazimwi ya majini. Afida anasema kuwa hiyo hali ya kukosa usingizi inampa mawazo ya kurudi motoni. Hii inaonyesha hali ya Afida kutoridhishwa na maisha ya Peponi.

Mwandishi pia ametumia mbinu hii kuonyesha tofauti zilizoko kati ya maisha ya Peponi na Motoni. Afida anakumbuka jinsi marehemu babake alikuwa akiwaleta pamoja na kuwaeleza jinsi wanavyofaa kuchukulia maisha. Anakumbuka jinsi babake alikuwa akiwasomea kitabu cha dini kila siku ya ijumaa. Anaeleza jinsi baba yake alivyokuwa akiwapa nasaha watoto wake na watoto wa jirani. Afida anadai kuwa kinyume na wa Peponi wa Motoni wana ushirika.

Ametumia mbinu hii kueleza tofauti zilizoko baina ya Peponi na Motoni. Anaeleza tofauti katika utamaduni, dini, malezi na maisha ya mtu kwa jumla. Ametumia mbinu hii pia kuonyesha jinsi Afida anavyotatizwa na vile mambo yalivyo Peponi. Anasema kuwa yeye, kinyume na wa peponi alifundishwa kutojibu kwa kutumia maneno yanayokera. Anakumbuka mara kwa mara jinsi wazazi wake walivyomlea. Hata Shuhuda rafikiye anapomshawishi kuwa akae kama wa peponi yeye anasisitiza kuwa lazima azingatie utamaduni wa kwao ambao unafaa kumwongoza

hata akiwa Peponi.

Katika sehemu ya kwanza ya sura hii tumengalia mbinu mbalimbali ambazo mwandishi ametumia kuendeleza maudhui katika *mhanga nafsi yangu*. Katika sehemu ya pili ya sura hii, tutaangalia jinsi mwandishi ametumia ukiushi wa kanuni za upole kujenga na kuendeleza maudhui katika riwya hii.

### **3.1.10 Ukiukaji wa kanuni za upole**

Ukiukaji wa kanuni za upole ni matumizi ya lugha bila kuzingatia kanuni na mikakati ya upole. Brown na Levinson (1978) ambao ndio waasisi wa nadharia hii wanadai kuwa mtu anapozungumza anafaa kuwa mwangalifu asimuudhi au kumuaibishi msikilizaji. Wanasema uso hasi na uso chanya wa msikilizaji unafaa kuhifadhiwa. Grice (1975) ambaye aliidara nadharia ya upole aliweka kanuni nne ambazo msemaji anafaa kuzingatia katika mawasiliano. Kanuni hizi alizitaja kama, kanuni ya kiasi, ubora, uhusiano na kanuni ya namna.

Kanuni ya kiasi inasema kuwa mtu anapozungumza asitumie maneno mengi ambayo hayaongezi umuhimu wowote kwa anayosema. Kanuni ya upole inasema kuwa msemaji anafaa kusema jambo ambalo ana uhakika nalo na wala asiseme jambo ambalo hawezi kulithibitisha. Kanuni ya uhusiano inasema kuwa unaposema usiseme mambo ambayo hayahusiani na mambo yanayojadiliwa. Kwa mfano ikiwa ni jambo la elimu linalozungumziwa usilete masuala ya umaskini. Nayo kanuni ya namna yasema kuwa jambo linalosemwa liwe wazi na msikilizaji asikisie anachoambiwa.

Katika sehemu hii tutachunguza jinsi mwandishi alivyokiuka kanuni hizi na jinsi ukiushi huu umesaidia kujenga na kuendeleza maudhui katika *Mhanga Nafsi Yangu*. Katika sura ya tatu tulitaja kuwa watu wa ukoo wa Afida walikuwa na matumaini makubwa sana kuwa Afida atakapofika Peponi atafanikiwa na atawatimizia mahitaji yao. Mwandishi ametumia ukiushi kwa kumtumia Bi Zaina. Kulingana na kanuni za upole za Grice (1975) Kanuni ya kiasi imekiukwa. Kanuni ya kiasi husema kuwa mzungumzaji asitumie maneno mengi ambayo hayaongezi maana zaidi kwa yanayosemwa. Bi Zaina badala ya kumwambia Afida angependa kuwekwa meno anasema mambo mengi mpaka Afida anachoka kumsikiliza. Kuchoka kwa Afida kunajitokeza kutokana na maneno ambayo mwandishi ametumia kuonyesha mawazo ya Afida alipokuwa akimsikiliza, "basi husemi nikuletee pesa utie meno hapa hapa petu Motoni? Sharti uje peponi?"

Unadhani nikifika huko tu nitajaza magunia kwa magunia ya pesa za kukuletea au kukununulia wewe vitu unavyotaka? Kweli peponi lakini..... Mwandishi anatangulia kwa kusema kuwa kila wakati Bi Zaina alirudia maneno yale yale.

"Ukishatulia huko Peponi usisahau kuniletea tiketi nje nitie meno. Si unaona hivi ubogoyo ulivyonitawala na kuniumbua sura. Sina hata jino moja la kutilia pozi. Hapa nilipo sina hata senti moja. Si unajua?"

"Alafu nikishatiwa meno na kurudi hapa nyumbani uniletee dala mia tano nataka kutia bati hili banda langu."

Katika mazungumzo ya Afida na Bi Zaina mwandishi anatumia ukiushi wa kanuni ya kiasi kuonyesha matumaini makubwa aliyokuwa nayo Bi Zaina. Bi Zaina hamalizii maneno yake kwa kusema apewe pesa za kuweka bati banda lake. Anamwambia Afida kuwa akishatia meno atampiku kwa uzuri na wanaume watampapatikia. Anaeleza pia kuwa akishatia bati nyumba, ataalika ndege wazuri kuja kutua juu ya paa. Bi zaina anasema maneno haya baada ya Afida kumwambia kuwa anataka kuweka bati ili avute bwana mpya, maana siku hizi wanaume hutafuta paliponona na wala hawatafuti sura njema na ujana. Aliyoyasema Bi Zaina kwa muda wa kama saa moja ni jambo ambalo angesema kwa hata dakika kumi. Ukweli ni kwamba maneno yakiwa mengi sana na yawe si muhimu msikilizaji anaweza kuchoka kusikiliza na akose hamu ya kusikiliza zaidi.

Katika majibu ya Afida kwa Bi Zaina mwandishi ametumia ukiushi kwa sababu majibu ya Afida kwa Bi Zaina pale aliposema anataka kutia meno hayakumfurahisha Bi Zaina. Ukweli ni kwamba hata katika hali halisia, alivyomjibu Bi Zaina haifai kwa sababu ya tofauti katika umri wao. Afida hakujali kuwa Bi Zaina alikuwa mzee kwa hivyo alistahili kujibiwa kwa heshima. Hakujali kuhifadhi uso hasi wa Bi Zaina. Kama tulivyotaja awali nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) msemaji anafaa kuwa mwangalifu asimudhi msikilizaji. Kulingana na msimulizi Bi Zaina hakufurahishwa na maneno ya Afida.

Katika kaida za jamii ya waafrika kuna mzaha ambao huwezi kumfanyia mtu aliyekupita kwa umri. Majibu ya Afida kwa Bi Zaina yalikiuka kanuni za kaida za jamii.

"Ama kweli unataka ujana mke

mwenzangu...' alitamka Afida waziwazi.  
Naona Ubogoyo huutaki ingawa wakati  
umeshafika, umechaga kutia meno...Aaa  
haya nimeyasikia nitatekeleza ombi  
lako..."Uk. 7

Maneno haya hata kama yalikuwa ya kweli Afida angeyasema kwa kutumia mkakati wa upole ambao ungemsaidia kumwambia Bi Zaina kuwa umri wake ulimruhusu kuwa kibogoyo. Mwandishi pia amemtumia Bi Sinangoa kuendeleza maudhui ya matumaini. Bi Sinangoa alikuwa shangazi ya Afida na alitarajia kuwa Afida angemkumbuka kwa sababu alipokuwa mdogo alikuwa akimpa chakula na hata wakati mwingine alimnunulia boflo. Bi Sinangoa alikuwa na shida ya tumbo ambalo lilikuwa limemsumbua kwa muda mrefu. Alikuwa na matumaini kuwa Afida afikapo Peponi atakuja kumchukua ili aende peponi kutibiwa. Katika mawasiliano haya, kuna ukiushi wa kanuni ya kiasi, kanuni ya namna na pia Bi Sinangoa ametumia lugha ambayo haikuhifadhi uso hasi wa wasikilizaji wake.

Ukiushi wa kiasi na namna umetokana na maneno mengi ambayo ametumia kueleza Afida kuwa angependa kwenda peponi kutibiwa. Anaeleza jinsi ambavyo ametibiwa na madaktari wengi

"Limewesha waganga tumbo hili. Limebwia gunia nzima la miti shamba, limekunywa chupa baada ya chupa za makombe yaliyoandikwa kwa sura nzito nzito za kur'ani. Limepuliwa na kuchuliwa kwa mafuta y auto na wachuaji wenye ujuzi kamili. Wapi! Anayeumwa kaumwa wenzangu hachagui dawa aumwaye wala hasiti kutafuta nafuu. Limemaliza hospitali tumbo hili na madakitari wake wazito wazito. Nikwambie nini? Sikupimwa huko kusipokwisha mara presha, mara mapigo ya moyo na mhemko, mara choo kidogo mara kikubwa, mara damu, mara makohoo, mara wapi sijui kutolewa maji na jizo tembe nazo je? Vipaketi kwa vipaketi kisha dawa za maji kwa vijiko vya chain a vya kulia au vikombe vya kahawa na gilasi. Usitaje sindano! Sijui ngapi nilizodungwa. Hivi nikuambiavyo makalio yangu yanawaka moto. Na madrip hayo, na kusaidiwa pumzi huko. Mradi limemaliza tumbo..."Uk 9

Bi sinangoa kwa kueleza haya yote alionyesha matumaini kuwa hata kama hawa wote walishindwa madaktari wa peponi wataweza wakati Afida atampeleka huko. Bi Sinangoa aliingiza mambo mengi katika ombi lake kwa Afida. Madaktari wa Motoni akawaita wezi. Mashehe akasema hawana maana tena na wala mungu hapokei dua zao. Watu walipocheka kwa sababu ya maneno yake aliwajibu kwa hasira na kwa kuwa palikuwa na watoto aliwaambia watu waliokuwa pale kuwa wanafuata tabia za watoto wao ambao hawakufunzwa adabu.

"Alaa! Mnacheka? Enh mnafuata watoto wenu wasiofundishwa baya? Haya shauri yenu mjue tu mcheka kilema hafi hadi kimfike. Yasiyomfika..." uk. 10

Kuwaambia watu wazima kuwa wanafuata tabia za watoto wao ambao hawajafundishwa baya ni kuwatukana, na baya zaidi ni kuwa anawatukana mbele ya watoto hao. Bi sinangoa hakujali kuhifadhi nyuso za watu hao. Angetumia maneno bora zaidi kuonyesha kutoridhishwa na vicheko vya watu hao na watoto wao.

Kanuni ya kiasi imekiukwa kwa kutumia Bi sinangoa. Ametumia maneno mengi kusema jambo moja tu, yaani angependa kwenda kutibiwa Peponi. Baada ya maneno haya yote Bi Sinangoa anamalizia kwa kusema kuwa kwa kuwa Motoni si kama Peponi anahakika atapata matibabu yafaayo. Mamake Afida pia alitumia maneno mengi sana kueleza kuwa angependa anunuliwe magari ya kubeba mizigo. Alianza kwa kusema shida alizozipitia tangu babake Afida afe. Anasema kuwa mwili wake unauma kwa mzigo alioachiwa na babake Afida.

"Nataka uninunulie gari moja kubwa la kubebea mizigo na basi moja la kufanyia biashara ya kupakia abiria. Ukiniletea magari hayo sitakuwa na sababu tena ya kukutaka uniletee pesa kila mwezi. Nitajikomboa kwa kuchapa kazi na kumwaga jasho ..." Uk 14

Kanuni za upole za Grice (1975) zinasisitiza matumizi ya maneno machache ambayo yanajikita kwenye suala husika. Katika mawasiliano haya, ukiushi wa kanuni hizi umesaidia kuonyesha jinsi ukoo wa Afida una matumaini. Katika hali halisia mtu anapoagiza kitu au kufanyiwa jambo fulani anafaaa kuwacha nafasi kidogo ya jambo hilo kutowezekana. Bi Zaina, Bi Sinangoa na Bi Mwamda, mamake Afida hawaachi nafasi ya kutowezekana. Anazungumza na uhakika kuwa



Afida atakapofika Peponi atapata pesa chungu mzima na atawaletea vyote walivtoitisha.

Kama tulivyoeleza awali, kwa mujibu ya nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987), msemaji anafaa kutumia lugha ambayo haitamuudhi au kumkasirisha msikilizaji. Katika riwaya hii, mwandishi amekiuka kanuni hiyo ili kuendeleza maudhui ya maonevu na udhalilishaji.

Afida anapofika Peponi anaugua na kupelekwa hospitali. Pale hospitalini, Bi Marneti na daktari wanatumia lugha ambayo ingeudhi mtu yeyote. Shangazi yake Afida anasema kwamba Afida alikuwa mbumbumbu mzungu wa reli kwa kuwa alikuwa hajakaa sana pale Peponi. Kumwita Afida mbumbumbu ni kumwita mjinga sana. Kulingana na waasisi wa nadharia ya upole, mwandishi ametumia ukiushi kwa sababu maneno yaliyotumiwa na Bi Marneti yalikuwa ni matusi na hivyo Bi marneti hakuhifadhi uso hasi wa Afida. Kwa kutumia maneno haya alimdhaliisha Afida. Ikiwa haja yake ilikuwa kumwambia daktari kuwa Afida ni mgeni Peponi, angetumia maneno mazuri kama vile, hajakaa hapa sana kwa hivyo hajazoea mambo ya Peponi' badala ya kumwita mbumbumbu mzungu wa reli.

Daktari pia alimdhaliisha Afida kwa kumwambia kuwa Peponi watu hufa kwa homa tu kinyume na Motoni ambako watu hufa kwa malaria, kifua kikuu au AIDS. Maneno haya hayakuwa maneno mazuri kumwambia Afida lakini mwandishi anayatumia kuendeleza maudhui ya udhalilishaji. Maneno haya yanakusudia kumdunisha Afida. Mwandishi ametumia maneno ya kuudhi na kumdunisha Afida ili kuonyesha jinsi watu wa Peponi wanavyowadharau watu wa Motoni.

Bi Marneti na Bw Bawa wanapoteta kuhusu afida, wanatupiana maneno yanayoudhi. Bw Bawa anamwambia Bi Marneti kuwa wanaume na wanawake wa peponi hawana wivu na utoto kama alionao Bi Marneti. Maneno haya ambayo ni matusi yanadhaliisha na kudunisha watu wa motoni.

"...sisi wanaume wa Peponi na hata  
wanawake hatupendi wivu wa kipumbavu  
namna wako. Sisi huaminiana..." uk. 41

Katika mazungumzo hayo Bi Marneti anamwambia Bw. Bawa kuwa Afida anafaa kwenda shule. Bw Bawa anamuuliza Bi Marneti kama amelifikiria suala la pesa. Bi Marneti anakasirika na kumwambia mumewe kuwa yeye kila kitu kikitajwa husema kuwa hakuna pesa.

Kwa kumjibu, Bw Bawa anamwambia mkewe kuwa Peponi kumeendelea kwa sababu ya pesa na huduma za kibinafsi na kijamii. Anamkumbusha Bi Marneti kuwa kwao motoni hakuna kinachoendelea isipokuwa umasikini maradhi na omba omba.

"... Tazama kwenu Motoni, kule  
kunaendelea nini zaidi ya umaskini, maradhi  
na omba omba?"Uk 42

Kwa kutumia ukiushi mwandishi ameendeleza maudhui ya udhalilishaji. Maneno haya yanamuudhi Bi Marneti na hata yanazua ugomvi mwingine. Katika mawasiliano ya Bw Bawa na Bi Marneti, ni wazi kuwa hata kama Bw Bawa amemuoa Bi Marneti, bado anawadharau wa Motoni. Katika mawasiliano ya Bw. Bawa na Bi Marneti Bw. Bawa anatumia maneno ambayo yanamuudhi Bi marnetti. Hata kama anayoyasema Bw. Bawa yana ukweli angeyasema bila kutumia maneno ya kumdunisha mkewe.

Shuhuda hata kama ni mmotoni anamdhalilisha Afida. Afida anakasirishwa na maneno ya Shuhuda ambayo mara nyingi huwa ya kumkumbusha kuwa lazima akae kama mpeponi na atumie uzuri wake kutengeneza maisha yake Peponi. Wanapokutana na Saparato, Saparato anajaribu kuongea na Afida. Kwa kuwa Afida bado ana tabia za motoni, anajiheshimu na hataki uhusiano wowote na wanaume. Kwa sababu ya msimamo huu, Shuhuda anamcheka kwa dharau. Maneno ya Shuhuda kwa Afida yametumiwa kumdhalilisha Afida.

" unafikiri uko motoni hapa. Hapa upo  
Peponi bibi. Kila mtu ana uhuru wa kufanya  
apendavyo hapa. Usisahau kwamba wewe  
mwanamke na mwanamke lazima aonyeshe  
mwili wake kama anataka kufanikiwa."uk.  
73

Maneno haya ya shuhuda yalimudhi Afida lakini mwandishi amefaulu kuonyesha udhalilishaji wa mwanamke na hasa mwanamke wa Motoni akiwa Peponi. Shuhuda hakujali kuhifadhi uso wake na hata wa Afida kama inavyodai nadharia ya upole.

Afida alipoolewa na Neshboch, alikuwa na shida sana kwa sababu She-shaiza nduguye Neshboch hakumpenda. Mara kwa mara alikuwa akimdhalilisha kwa kumuuliza maswali ambayo yalikuwa yanamuudhi, sio Afida tu bali na wengine. Alikuwa anamuuliza maswali kama vile; "nasikia Saiwama wanakunywa damu. Nasikia mnapika lakini vyakula vyenu vina

mafuta mengi"

Swali la kwanza linakiuka kanuni za upole kwani swali kama hilo linaweza kuudhi mtu anayeulizwa. Kuuliza mtu kama kwao wanakunywa damu na kumwonyesha kuwa chakula chao si kizuri ni ukiushi wa upole kwa sababu ni maneno ambayo yanatumiwa ili kuudhi. Kulingana na nadharia ya upole ya Brown na Levinson mtu anapoongea anafaa kuhifadhi uso wa msikilizaji kwa kutumia maneno mazuri anapoongea. Afida aliudhika na hili lilidhihirishwa na majibu aliyotoa.

Mwandishi amefaulu kuendeleza maudhui ya udhalilishaji pale ambapo Afida na Neshboch wanapokosana. Neshboch, usiku mmoja anamfukuza Afida. Baada ya Afida kurudi maisha yanabadilika na ugomvi unakuwa ni jambo la kawaida. Siku moja Afida na Neshboch wanapogombana, Afida anafahamu kuwa hata kama Neshboch alimwoa anawadharau wa motoni sana.

"Chakula tayari mezani."

"Nani anayetaka kula chakula kichafu na kisicho thamani?"

"Leo hivyo, wewe si ndiye uliyekuwa ukiramba sahani kwa vidole na ulimi kwa chakula nilichokupikia? Si wewe uliyekuwa ukikisifu kila chakula ninachopika? Sasa kimezidi nini?"

"Nikiramba, nikiramba... hakukuwa kuramba kule kulikuwa kusafisha takataka tu za sahani tu?" Uk 168

Ugomvi huu unaendelea na Neshboch anamwambia Afida kuwa hamstahiki. Alizidi kumtupia matusi na kumwambia kwamba alikuwa mke wake alipokuwa na uchu na kwa kuwa uchu umeisha hana hamu tena. Anamwambia Afida kuwa alibahatika kuolewa naye kwa sababu wa-Motoni hawastahiki kuolewa na wa-peponi kwa sababu walikuwa watumwa wao.

"Wewe una bahati kwelikweli kuolewa nami, kwani nyinyi wa-Peponi hamstahiki kuolewa nasi. Mlikuwa watumwa wetu zamani." Uk. 169

Ugomvi huu uliendelea huku wakirushiana matusi ya kila namna. Afida anamwambia Neshboch

kuwa kauli yake ya kuwa walikuwa watumwa wao na hivyo hawawastahiki imepitwa na wakati Neshboch anamuuliza Afida anajua nini kuhusu wakati. Anamwambia kuwa kama angejua maana ya wakati basi yeye na jamii yake wangukuwa sehemu ya binadamu. Afida anamwambia Neshboch kuwa yeye ni binadamu kuliko yeye. Mwishowe Neshboch anamwambia Afida kuwa hafai kumjibu vibaya kwa sababu alimuokota njiani. Hata kama Afida hana tabia ya kutukana, Neshboch anamsukuma mpaka anamjibu kwa matusi. Neshboch alipomwambia Afida kuwa alimuokota njiani anamjibu kwa kumtusi;

"Ikiwa umeniokota njiani, basi huna akili wewe, maana umejikubalisha kuzoa na kutia takataka na uchafu nyumbani mwako" uk  
169

Maneno ya Neshboch katika ugomvi huu yanaonyesha wazi jinsi wa-Peponi wanavyowadharau wa-Motoni. Neshboch ametumia maneno ya kumtusi na kumdhalilisha Afida. Anamkumbusha kuwa wa-Motoni walikuwa watumwa wao na hawastahili kuwekwa katika kikundi cha watu.

Kulingana na nadharia ya upole, mawasiliano yanafaa kuendelezwa kwa njia nzuri ambayo msemaji na msikilizaji wanaelewana. Uso hasi wa msemaji na msikilizaji unafaa kuhifadhiwa. Msikilizaji hafai kuudhiwa au kuaibishwa. Ukiushi huu umeendeleza maudhui ya maonevu na udhalilishaji kikamilifu. Kama msimulizi angetumia maneno yake kueleza jinsi wa-Motoni wanavyodhalilishwa wakiwa Peponi, maudhui hayangetokea vizuri kama yanavyotokea kwa kutumia ukiushi wa kanuni za upole.

Kama tulivyosema awali, swala la upole ni la kijamii. Katika jamii ya waafrika, swala la mapenzi halijadiliwi waziwazi hadharani na pia halijadiliwi mahali ambapo kuna watoto. Katika riwaya hii, mwandishi amekiuka kanuni hii. Katika uwanja wa ndege, Bi Zaina na Afida wamezungumzia sana swala la mapenzi. Afida anamwambia Bi Zainabu kuwa anataka kuweka bati ili amvute bwana mpya. Kawaida utani kama huu haufai kwani Afida ni mtoto sana kutaniana na Bi. Zainabu. Mwandishi ametumia ukiushi huu kuendeleza maudhui ya furaha yaliyokuwa pale katika uwanja wa ndege.

Mwandishi katika usimulizi wake pia amekiuka kanuni za upole za kijamii anapoeleza matukio katika hospitali pale Afida anapojulishwa kuwa Shuhuda alikuwa hali mahututi. Kawaida huwezi kusema waziwazi kuwa mtu yuko karibu kufa. Mwuguzi anapoenda kumwita Afida akamwone

Shuhuda, anamwambia kuwa kuwa Shuhuda yuko karibu kufa.

"Kumezidi nini tena?" aliuliza Afida.  
"Nadhani yuko katika hatua zake za  
mwisho- karibu... Karibu ataaga" uk. 187

Usimulizi wa mwandishi katika kueleza hali ya Shuhuda pale hospitalini unakiuka kanuni za upole. Kawaida huwezi kueleza hali ya mgonjwa kwa maneno aliyoyatumia mwandishi. Mwandishi anaeleza kuwa Afida alikuwa amelala mlalo wa kujikunyata na kujipinda kama korosho, Shuhuda alikuwa kama mzigo mtupu.....mzigo wa mifupa uliotupwa kitandani kama vile hauna mpagazi wa kuubeba. Anaendelea kueleza kuwa mzigo huo ulikuwa umechomekwa macho makubwa meupe na pua iliyobaki kitojo regerege kwenye maego dhaifu yaliyopoteza nyama usoni pake. Mwandishi ametumia maneno mengi ambayo angeyasema kwa maneno mawili au matatu yaani, "Shuhuda alikuwa amekonda na kukondeana." Kwa kutumia ukiushi huu, mwandishi ameweka wazi picha halisi ya Shuhuda wa sasa na Shuhuda wa zama zile alipokuwa msichana. Picha hii pia inaonyesha jinsi maisha ya Peponi yanavyoweza kuishia vibaya. Maisha aliyokuwa anaishi Shuhuda na uzuri aliokuwa nao hangefikiri kuwa atakufa hivyo.

### **3.2. HITIMISHO**

Katika sura hii tuna sehemu mbili. Katika sehemu ya kwanza tumeangalia matumizi ya lugha ambayo mwandishi ametumia kuendeleza maudhui katika *Mhanga Nafsi Yangu*. Katika sehemu ya pili tumeangalia jinsi mwandishi ametumia ukiushi wa kanuni za upole kuendeleza maudhui katika riwaya hii. Katika sehemu ya kwanza tumeona ya kwamba mwandishi ametumia mbinu mbalimbali kama vile tashbihi, takriri, methali, misemo mbinu rejeshi na nyinginezo. Kwa kutumia mbinu hizi, mwandishi ameendeleza maudhui ya udhalilishaji, ubaguzi, unyanyasaji, unafiki na mengineyo.

Katika sehemu ya pili tumeangalia jinsi ukiukaji wa kanuni za upole umetumiwa kujenga na kuendeleza maudhui kwa kutumia nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) na kanuni za upole za Grice (1975). Tumeangalia jinsi mwandishi ametumia lugha inayokiuka kanuni za upole kuendeleza maudhui makuu na dhamira kuu ya riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*.

## SURA YA NNE

### MAUDHUI KATIKA *MHANGA NAFSI YANGU*

#### 4.0 Utangulizi

Katika Mhanga Nafsi Yangu maudhui makuu ni ya matumaini, ubaguzi, udhalilishaji, maonevu na dhulma. Ili kuendeleza maudhui haya mwandishi amemtumia mhusika mkuu Afida. Afida ametumiwa kusimamia jamii nzima ya watu weusi wakiwa nchi za ng`ambo.

Katika sura hii tumeangalia jinsi mwandishi ameendeleza baadhi ya maudhui kwa kutumia ukiushi wa upole.

#### 4.1 SINOPSIA YA *MHANGA NAFSI YANGU*

*Mhanga Nafsi Yangu* ni riwaya ambayo inaangazia jinsi jamii huchukulia suala la kuenda nchi za ng`ambo. Mwandishi anaangazia mawazo ambayo waafrika huwa nayo kuhusu maisha ya nchi za ng`ambo. Anaangazia jinsi maisha ya ugaibuni yanavyoweza kumbadilisha mtu na hata kusahau mila na desturi za kwao.

Amefaulu kuonyesha kuwa kinyume na wanavyofikiria watu, maisha ya ugaibuni si lazima yawe mazuri bali kuna panda shuka za maisha kwa jumla. Katika riwaya hii mhusika mkuu ni msichana anayeitwa Afida aliyebahatika kwenda peponi', kama mwandishi anavyokuita katika riwaya hii. Afida anaenda Peponi kwa mwaliko wa shangazi yake Bi. Marnetti. Watu wa ukoo wamefurahi sana kwa sababu wanaamini kuwa Afida akienda Peponi atawamalizia umaskini. Vitu wanavyoitisha ni dhihirisho kwamba wanatarajia pesa nyingi sana kutoka kwa Afida. Kwa mfano mama yake Afida anaitisha lori moja na basi la kubebea abiria. Afida afikapo Peponi anakumbana na shida chungu nzima. Kwanza kabisa anakumbana na matatizo nyumbani kwa shangaziye kwa sababu shangaziye Bi Marnetti anamuona kama tishio kwa ndoa yake. Anamwambia Afida aepuke kumwangalia mumewe kwa macho ya mwani. Bi Marnetti wanakosana na mumuwe kwa sababu ya Afida na wanaamua aende chuo ambako atakaa kwa nyumba yake.

Afida anapohamia huko nje anakumbana na matatizo vilevile. Shuleni walimu na wanafunzi wanambagua kwa misingi ya rangi. Wanamuuliza maswali ambayo lengo lake ni kumdhalilisha. Afida anaishi maisha ya upweke na huzuni na mara kwa mara anajikuta analia.

Kwa muda Afida ameweza kudumisha tabia yake nzuri mpaka pale anapokutana na Shuhuda. Shuhuda ni m-Motoni ambaye amekaa Motoni kwa muda mrefu. Anajaribu kumuonyesha Afida maisha ya Peponi lakini hafaulu. Baada ya muda Bi Marnetti anamshawishi Afida aolewa na mzee ambaye alikuwa amempita kwa umri sana. Bi Marnetti anataka Afida aolewe na huyo mzee ili wapatao mtoto amchukue kwa sababu alikuwa tasa. Uhusiano wake na Bi marnetti pia ulikuwa mzuri lakini ukazoroteka pale ambapo Afida alipokataa kupeana mtoto wake.

Afida aliweza kukaa vizuri kwa kuzingatia maadili na utamaduni wao hadi pale ambapo alipopokonywa mtoto wake na mahakama kwenye kesi iliyowasilishwa na mumewe. Baada ya kugombana na mumewe Neshboch, alipewa talaka na korti ikaamuru mumewe apewe mtoto. Aliendelea kukaa na mtoto hadi pale ambapo Neshboch, Sheshaiza na Bi. Marnetti walipopanga jama ya kumpokonya. Walifaulu kumsingizia kuwa ni mlevi kupindukia na ameshindwa kumlea mtoto wake. Korti iliamuru kuwa mtoto achukuliwe. Baada ya kupokonywa mtoto Afida aliamua kuwa ikiwa amepokonywa mtoto kwa kusingiziwa ulevi basi atakunywa hiyo pombe kupindukia. Kuanzia hapo Afida alibadilika na maisha yake yakawa ni ya pombe. Maisha hayo yalimpelekea kupata mtoto mwingine nje ya ndoa. Kwa sababu ya ugumu wa maisha kiuchumi, Afida alianza ukahaba ili aweze kulea mtoto. Aliharibika kiasi kwamba angejiuza hata kwa chupa moja ya pombe. Wakati huu wote Afida alikuwa amesahau Motoni na hata ahadi alizokuwa ameweka. Mpenzi wake Shabaan alijiua pale alipogundua kuwa Afida alikuwa ameivunja ahadi yao ya ndoa. Baada ya Shabaan kufa mwandishi hajaongea tena kuhusu ukoo wa Afida. Riwaya inaishia kwa mauti kwani Shuhuda anakufa kwa ugojwa wa ukimwi naye Afida hatima yake haijulikani hata kama mara ya mwisho aliposikika alikuwa mgojwa saratani ya fuko la uzazi.

#### **4.2 Ukiushi wa upole unavyoendeleza maudhui katika *Mhanga Nafsi Yangu*.**

Kwa kuwa tasnifu hii inakusaidia kuangalia jinsi ukiukaji wa kanuni za upole umetumiwa kujenga maudhui na kuboresha mtindo wa *Mhanga Nafsi Yangu*, tumengalia jinsi ukiushi wa upole umetumiwa kuendeleza maudhui makuu katika riwaya hii. Maudhui makuu katika riwaya hii ni matumaini, udhalilishaji, ubaguzi wa rangi, usaliti na mengineyo kama tutakavyoona. Kuna maudhui ya elimu, umaskini, utamduni na majuto hata kama hayajajengeka sana.

##### **4.2.1 Wasiwasi**

Katika riwaya hii kuna maudhui ya wasiwasi. Afida anaposafiri kwenda peponi anakumbwa na

mawazo chungu mzima. Hata akiwa ndegeni kuelekea peponi bado haamini anaenda. Kulingana na msimulizi Afida haoni raha kuwa mbali na motoni hata kama hakuna mazuri huko motoni.

"Haoni tamu kabisa Afida kuweko mbali na motoni, kule alikozaliwa na kukua...  
Ameingiwa na pumbao ambalo  
limemsahulisha umuhimu wa safari hii. Uk 3

Kulingana na msimulizi, si ajabu Afida kuwa na wasiwasi kwani safari hii inaweza kubadilisha maisha yake kwa namna nzuri au mbaya.

Katika hali halisi, mtu anoposafiri kwenda ugenini ni kawaida kuwa na wasiwasi kwani mtu huwa hana hakika na yale yanayomsubiri anakokwenda. Hii ndiyo hali ambayo alikumbwa nayo Afida. Yaliyomtia wasiwasi zaidi Afida ni tashwishi walizokuwa nazo vijana wenzake. Alikuwa na wasiwasi kuhusu jinsi peponi kulivyo, jinsi kutakavyompokea na hasa akikumbuka kuwa shangazi yake aliyemwita hajawahi rudi tangu alipoenda na ndio mara yake ya kwanza kusikika.

Mchumba wake Afida Shaabani pia alikuwa na wasiwasi walipokuwa wakiagana na Afida. Hata kama Afida alikuwa na wasiwasi na huzuni wa kuachana na mpenzi wake, Shaabani alionyesha wasiwasi wake kwa kumwomba Afida asimsahau na anapoongea analia.

"Ninalokuomba...au ninalokuagiza mimi ni kumbukizi zako tu. Usinisahau na usisahau mapenzi yetu." Uk. 15

#### **4.2.2 Matumaini**

Ukoo wa Afida una matumaini makubwa kuwa Afida akienda peponi shida zao zitakwisha. Maudhui haya yanajitokeza pale ambapo ukoo wa Afida unapomsindikiza kwenye uwanja wa ndege. Kuna wale wana matumaini ya kuletewa vitu, wengine wanatarajia kumfuata Afida huko Peponi ili kufanyiwa jambo hili na lile.

Baadhi ya walio na matumaini makubwa ni bibi yake Afida aliyeitwa Bi Zaina. Yeye alimtaka Afida amtumie tiketi ili aende peponi akatie meno kwani ni kibogoyo, pia alitaka akirudi kutoka peponi kutia meno atumiwe pesa, za kuweka bati nyumba yake. Bi Zaina alikuwa na matumaini kuwa Afida akifika peponi atapata pesa nyingi ambazo zitamwezesha kulipia tiketi ya kwenda huko, kugharamia kutiwa meno na hata kumpa pesa za kugharamia ukarabati wa nyumba yake.



Mwengine aliyekuwa na matumaini ni Bi Sinangoa ambaye alikuwa shangazi yake Afida. Bi Sinangoa alikuwa na shida ya tumbo ambalo lilikuwa limemsumbua kwa muda mrefu. Alitaka kwenda peponi kutibiwa huko pale tu Afida atakapotulia.

"Bi Mdogo , Fanya juu chini fanya  
utakayoweza huko uendako unitengenezee  
safari...nipate matibabu ya mtumbo  
huu."Uk. 15

Mamake Afida pia ana matumaini makubwa kuwa bintiye atafanikiwa. Alimwagiza Afida amnunulie magari mawili makubwa moja la kubebea mizigo na jingine la kubeba abiria. Kulingana na mamake Afida magari hayo yatamsaidia kuondoa umaskini nyumbani kwao. Vile Vile alikuwa na matumaini kuwa Afida angerudi siku moja.

Shaabahi mchumbaye Afida pia alikuwa na matumaini kuwa Afida angerudi na wangepunga ndoa. Anamwambia Afida, "usilie Afida, mungu akipenda tutakutana tena kutekeleza ahadi yetu ya ndoa."

Katika kuendeleza maudhui haya, mwandishi ametumia ukiukaji wa kanuni za upole Grice (1975), anapendekeza kanuni nne za ushirikiano katika mazungumzo yoyote. Kanuni hizi ni kanuni ya ubora, kanuni ya idadi, kanuni ya uhusiano na kanuni ya namna. Katika kuendeleza maudhui ya matumaini kanuni ya idadi, ubora na uhusiano zimekiukwa. Kanuni ya idadi inasema kuwa mtu anafaa kusema mambo ambayo yanahitajika tu na wala asitumie maneno mengi ambayo si muhimu.

Katika uwanja wa ndege ukoo wa Afida unapomsindikiza, Bi Zaina anatumia maneno mengi ambayo si muhimu. Katika mazungumzo ya Afida na Bi. Zaina, ukiushi wa kanuni ya idadi umetumiwa kuonyesha matumaini makubwa aliyokuwa nayo Bi Zaina.

Badala ya kusema angependa kwenda Peponi kutiwa meno, anaeleza Afida jinsi ubogoyo ulivyomtawala na hana hata jino la kutilia pozi. Anamwambia Afida kuwa akishatia meno atampiku kwa uzuri na wanaume watampapatikia. Maneno haya si muhimu hata kidogo tukizingatia kuwa Bi. Zaina ni mama ambaye amekomaa kiumri na hivyo hata kufikiria jinsi wanaume watakavyompatikia ni ajabu.

Mwandishi vile vile ametumia ukiushi wa kanuni za upole kwa misingi ya jamii. Kama

tulivyosema katika maelezo ya nadharia, kila jamii ina sheria zake ambazo huitawala. Katika jamii ya waafrika, masuala ya mahaba hayajadiliwi na watu walio na tofauti kubwa kiumri na hasa mbele za watoto. Afida na Bi. Zaina wanapojadili kuhusu ubogoyo, Bi. Zaina anamwambia Afida kuwa akishatiwa meno na kurudi Motoni anataka apewe pesa za kununua bati la kuweka kwenye banda lake. Afida anamtania bibi yake kwa kumwambia kuwa anataka aweke bati ili amvute bwana mpya.

Bi. Zaina kwa kumjibu Afida anamwambia kuwa anamwonea wivu kwa sababu akitia meno wanaume watampapatikia na akitia bati kwenye banda lake ataalika ndege wazuri kutua juu ya paa lake. Wazungumzo kama haya hayafai kuendelezwa na watu waliotofautiana umri lakini mwandishi ametumia maksudi ili kuonyesha furaha na matumaini waliokuwa nayo watu wa ukoo wa Afida.

Mwandishi pia ametumia ukiushi wa kanuni ya ubora ambayo inasema kuwa msemaji aseme jambo ambalo anaweza kuthibitisha ukweli wake. Amemtumia Bi. Sinangoa kuendeleza zaidi maudhui ya matumaini. Bi. Sinangoa bali na kutumia maneno mengi kusema jambo moja amesema mambo ambayo hana uhakika nayo. Bi. Sinangoa anamwambia Afida kuwa angependa kwenda Peponi kutibiwa tumbo lake ambalo limemsumbua kwa muda mrefu. Badala ya kumwambia hivyo moja kwa moja, anaanza kwa kueleza jinsi utumbo huo umemsumbua na jinsi ametibiwa na madaktari wengi. Anaeleza jinsi amekunywa chupa nyingi za dawa za chumba na za miti shamba, jinsi tumbo hilo huchuliwa na wachuaji hodari na jinsi hata makalio yake yanauma kwa sindano. Jambo ambalo angesema kwa dakika moja analisema kwa zaidi ya nusu saa.

Baada ya kusema maneno hayo yote, Bi Sinangoa anasema kuwa motoni madaktari wameisha na hata mashehe hakuna. Anasema kuwa hata kama kuna mashehe, siku hizi hata wakikusomea dua hazifiki kwa mungu na wala mungu hazipokei dua za mashehe hao.

Kulingana na kanuni ya ubora, huu ni ukiushi kwa sababu hata kama Bi Sinangoa alikuwa ametibiwa na madaktari wengi bila kupona, si kweli kuwa hakuna madaktari Motoni. Vile vile, kusema kuwa hakuna mashehe tena na hata kama wako mungu hapokei dua zao pia si kweli. Mwandishi ametumia ukiushi huu kuonyesha matumaini aliyokuwa nayo Bi Sinangoa kuwa akienda Peponi atapata daktari mzuri wa kutibu tumbo lake.

### 4.2.3 Maovevu na dhulma

Katika riwaya hii maudhui ya maonevu kwa wanawake yanajitokeza. Nafasi ya mwanamke katika jamii ni duni. Maudhui haya yanajitokeza kutokana na Afida ambaye kulingana na mwandishi alikuwa akijisaili mara kwa mara kwa nini alizaliwa mwanamke. Katika ndoto Afida anaona mwanamke akiwa na upungufu wa maisha kinyume na mwanaume ambaye mara tu anapozaliwa hupewa nafasi ya kuishi maisha kamili

"..... mtu akizaliwa mwanamke hana haki ya kuishi kiutotonofu duniani....anabaki tu zumbukuku....."Uk. 17

Katika fikra zake anaasema kuwa anayetaka kuwepo lazima ajijengee ngome ya kuwepo. Anasema kuwa yeye aliamua kujijengea ngome ili awepo hata kama alijua kuwa jamii ingembana na kumzuia asichukue hatua yoyote kwa kuwa yeye ni mwanamke.

Kuna maudhui ya dhulma. Afida anapofika peponi, chumba anacholala kina baridi kiasi kwamba hapati usingizi vizuri. Shangazi yake na mume wake wanalala kwenye chumba kikubwa kilichojaa uvuguvugu. Analinganisha chumba anacholala na chumba cha maiti. Afida analazimishwa kutoka nje hata wakati hataki. Afida anasema kuwa ana maswali mengi sana yanayohitaji majibu lakini hawezi kuyajibu kwa sababu hajawa yeye.

"...mpaka sasa anajua kwamba hawezi kuyajibu...hajawa yeye yaani mtu mwenye uhuru wake hapa peponi."Uk 17

Shangazi yake Afida pia alisisitiza kuwa Afida alazwe chumba chenye baridi ili azoe na pia alale mbali na chumba chake na mumewe ili apelelezwe kama ana maradhi. Maisha ya Afida yamejaa dhulma kwani hata kule kupokonywa mtoto ilikuwa ni kudhulumiwa kwa sababu yeye ni mweusi na mweusi hana haki Peponi.

### 4.2.4 Tuhuma

Kuna maudhui ya tuhuma. Bi Marneti kwa muda mfupi ambao amekaa na Afida, ameanza kumshuku kuwa anaweza kumchukulia mume wake. Ni dhahiri pia kuwa Bi Marneti hamwamini mumewe kwa sababu kama angemwamini hangemdhania kuwa Afida anaweza kuwa na uhusiano wa kimapenzi na yeye. Kuendeleza maudhui haya mwandishi ametumia ukiushi wa kanuni za upole. Nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987), inasema kuwa msemaji hafai kutumia maneno ambayo yanaweza kumuudhi au kumuabisha mtu. Maneno ya Bi. Marneti

anapomwonya Afida asimwangelie mumewe kwa macho ya mwani yanamshangaza na kumuudhi. Anashangaa vipi Bi. Marneti anaweza kumwambia maneno kama hayo.

Afida anasema kuwa kwao Motoni mtu angeshangazwa na maneno ya Bi. Marneti kwa sababu ya tofauti ya umri baina yake na Afida. Kulingana na Afida maneno ya Bi. Marneti ni utovu wa adabu. Kulingana na nadharia ya upole huu ni ukiushi kwa sababu kama Afida anavyosema ni mwiko katika jamii kwa mama kama Bi. Marneti kuongea na Afida kuhusu kupokonyana mume. Nadharia ya upole inasema kuwa kila jamii ina miiko yake na inapovunjwa kama alivyofanya Bi. Marneti, huo ni ukiushi. Kwa kutumia ukiushi huu mwandishi amefaulu kuonyesha jinsi Afida alivyokumbana na masaibu mara tu alipofika Peponi.

#### **4.2.5 Udhalilishaji**

Kuna udhalilishaji ambao unadhihirishwa kupitia Afida. Afida anapopelekwa hospitalini shangazi yake anaeleza daktari kuwa Afida hajazoea baridi na pia haelewi mambo ya ma-heater'.

".....unajua mambo haya ya ma-heater hayako Afrika. Na yeye kaja hapa juzi tu, mbumbumbu mzungu wa reli!" Uk 37

Kujibu, daktari anaeleza Afida kuwa anastahili kujikinga na baridi kwa sababu kuna virusi ambavyo vingempa mafua mabaya

Anamweleza kuwa watu peponi hufa kwa mafua kama vile wao hufa kwa malaria, kifua kikuu au AIDS

".....watu wengine hufa kwa mafua hapa kama mnavyokufa nyinyi kwa malaria ,kifua kikuu au AIDS mafua hapa....."Uk 37

Udhalilishaji pia unadhihirika nyumbani kwa Bi Marneti pale ambapo Afida anapotaka kukoga. Bi Marneti anamwambia kuwa hata akikoga mara milioni hawezi kuwa mweupe kama wa-Peponi. Bi Marneti pia anadhalilishwa na mumewe kwa kuambiwa kuwa peponi mambo huenda vizuri kwa misingi ya pesa lakini motoni kinachoendelea ni umaskini, maradhi na ombaomba.

".....Tazama kwenu motoni, kule kunaendelea nini zaidi ya umaskini, maradhi na ombaomba?" Uk 37

Afida alipoenda kusoma, walimu na wanafunzi wengine walimdharau kwa misingi ya rangi. Kila

wakati walimu walikuwa wakimuuliza kama kipeponi ni kigumu ili wadhibitisha kuwa wa-Peponi wana akili nyingi kuliko wa Motoni. Kulingana na wa-Peponi ikiwa unaweza kuongea lugha yao basi una akili nyingi kuliko wa-Peponi hata kama ndio lugha yako asilia. Unashangaa kwanini wanatarajia wewe ujue lugha yao na wao hawawezi kuongea yako hata neno moja.

Shuhuda ambaye ni wa kutoka motoni lakini amekaa Peponi kwa muda mrefu anamdharau Afida. Alikuwa anamwita mshamba kwa sababu alikuwa amekataa kubadilisha mavazi yake na kuvaa kama wa-Peponi.

Maneno ya daktari kwa Afida kuwa Motoni watu Motoni hufa kwa magonjwa yale mabaya kinyume na Peponi ni udhalilishaji wa waafrika kwa jumla. Haya ni matusi na nadharia ya upole inasema kuwa msemaji anafaa kuhifadhi uso wa msikilizaji ili aepuke kumuuthi au kumuaibisha. Vile vile maneno ya Bw. Bawa kwa mkewe kuwa Motoni hakuna kinachoenedelea ila magonjwa, umaskini na ombaomba ni matusi. Maneno haya yametumiwa kuonyesha jinsi watu wa Peponi wanavyowadharau watu wa Motoni.

Mwandishi angetumia usimulizi kueleza kuwa watu wa Peponi ni maskini, wajinga na huugua magojwa mabaya kulingana na watu wa huko lakini ameamua kutumia ukiushi ili kuyajenga maudhui. Maneno wanayoyatumie watu tuliotaja yanatoa picha ya wazungu wanavyowaona waafrika.

#### **4.2.6 Huzuni**

Kuna maudhui ya huzuni. Hali ya huzuni inadhihirika hata kabla Afida hajatoka Motoni. Mamake Afida analia anapomwaga mwanawe na hata Afida mwenyewe analia. Shabaan ana huzuni anapomwaga mpenziwe Afida. Afida anapofika peponi, maisha yake yanaaza kwa huzuni kutokana na kelele na maonevu ya shangazi yake. Afida anaeleza jinsi anavyolia mara kwa mara. Huzuni ya Afida inatokana sana na ile hali ambayo shangazi yake amemweka kwa chumba chenye baridi na pia kwa kumwambia kuwa anamnyemelea mume wako.

".....Hapo tena nikajikuta nabubujikwa  
na machozi mashavuni rovurovu  
nikabaki kulia kwa kwikwi na  
kekefu....." uk 43

".....Sikujua kwa nini. Labda nilihisi  
taabu kutazama jinsi nilivyo, nililia

machozi njia mbili." Uk 43

Afida anaeleza kuwa wakati mwingi alitaka kutoka pale nyumbani ili aondokee Bi. Marneti kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa chanzo cha huzuni yake

Bali na huzuni iliyoletwa na mateso ya Bi Marneti, Afida alipigwa na mbiwi la huzuni alipojua kwamba mpenziwe Shabaan alikuwa amekufa. Shabaan mwenyewe pia kabla ya kifo chake alikuwa na huzuni kwa kuwa Afida alikuwa hajibu barua zake.

Afida alihuzunika pia pale ambapo Shabaan alimpigia simu. Shabaan alipiga simu akiwa hali mahututi. Afida anaeleza jinsi alivyozungumza na Shabaan na kusikia sauti ya kudhoofika iliyoonyesha wazi kuwa Shabaan alikuwa mgonjwa sana.

".....nini cha mno?" sauti yangu ilikuwa imejaa pumzi za huzuni na huruma . Uk. 86

Maisha ya Afida peponi yalisheheni huzuni kwani mwisho kabisa alihuzunishwa zaidi na kifo cha rafiki yake Shuhuda aliyekufia peponi kutokana na ugonjwa wa ukimwi.

Riwaya yenyewe inaishia kwa huzuni kwa sababu hatima ya Afida haijulikani. Mtoto wake mkombozi alipelekwa kwa polisi pale ambapo Afida alipolazwa hospitali kwa ugonjwa wa saratani ya fuko la uzazi.

#### **4.2.7 Uozo wa jamii**

Katika riwaya hii pia kuna uozo katika jamii. Kuna unyayasaji na walio navyo wanataka zaidi, tamaa huwafanya watu kuwa na roho ya unyama, kuna unyang'anyi, wizi, kuua na hata kuporomosha mabomu. Maudhui haya yanadhihirika kutokana na mazungumzo ya Afida kwa nafsi yake. Anasema kuwa maovu haya watu hufanya ili kujifaidi wenyewe bila kujali watu wengine.

" .....kuiba tunaona ni jambo la kawaida tu, kunyang'anya ni mchezo tu, kuua hakuna hatia tunaweza mara moja kuchinja." Uk. 47

Uozo wa jamii pia unadhihirika pale Shuhuda anapoongea na Afida. Anamwambia kuwa peponi mtu ana uhuru wa kufanya anavyotaka. Anamkumbusha Afida ni mwanamke na hivyo akae kama mwanamke.

".....usisahau kwamba wewe mwanamke,  
na mwanamke lazima aonyeshe mwili wake  
kama anataka kufanikiwa." Uk. 73

Afida baada ya kukaa peponi alipata mtoto na Neshboch aliyekuwa mpeponi, Baada ya muda walitalikiana na Afida akapewa haki yake ya kumtunza mtoto wao. Neshboch alipanga njama na Afida akapokonywa mtoto kwa kusingiziwa kuwa hufika nyumbani mlevi na kumtesa mtoto wake. Pale mahakamani wakili wa Afida hakufika kumtetea kwa sababu wote walikuwa wamehongwa na Neshboch.

".....Afida alipigwa na mshangao  
mkubwa kwamba hata wakili wake  
ananunuliwa....." Uk. 73

Afida alipopokonywa mtoto, aliingilia ulevi kwa kukosa matumaini maishani kwa kuwa pesa alizokuwa nazo hazingeweza kutosha matumizi ya kila siku. Afida aliingilia maisha ya ukahaba. Ukahaba huwa ni dalili ya uozo wa jamii kwa kuwa wanaume na wanawake wote wanachangia katika uovu huu. Mwandishi anaeleza kuwa Afida alikuwa analala na mwanamume yeyote bora tu apate kitu kidogo.

".....Akabidi kuingia katika bwawa huria  
la kuogelea katika ngono" uk. 177

".....kwa nini kajiachilia namna  
hii.....uhuru wa kuuza ovyo mwili wake?  
kuuza kwa chupa moja tu ya bia." Uk. 179

#### **4.2.8 Unafiki**

Maudhui ya unafiki yanajitokeza katika riwaya hii. Afida anaeleza jinsi anavyopanda basi kila siku na kukutana na mama ambaye kila mara hugeuka kumwanguka. Kulingana na Afida, huyu mama hugeuka kumwanguka kwa sababu ni mwafrika. Afida anasema kuwa kila anapomtazama, yeye humtazama kwa jicho la kumdanganya .

"Lazima ukasirike moyoni na utabasamu  
machoni tu, kama si hivyo utapata jaka la  
moyo kwa hawa watu wanaochukia bila  
kusema....." uk. 63

Afida pia anasema kuwa hata kama mapenzi yake kwa Shabaan yamepungua angemwandikia barua hata kama ni ya kumdanganya ili aache kusononeka huko motoni.

".....Aaaa,kwa nini lakini siwezi kushika kalamu kumwandikia maneno mawili matatu yasiyo na maana lakini yanayotoja asali,ili angalau kumdanganya na kumtia tamaa tu?.....lazima adanganywe kama mtoto mdogo....." uk 69

Unafiki pia unaonekana pale ambapo separato anapokutana na Afida na Shuhuda.Kila wakati Separato alijifanya mzuri kwa kutaka kulipa bili wakati wowote walipokutana. Separato hakuwa anafanya hivyo bure, alilipa bili kwa sababu alimtaka Afida na Afida alikuwa anaelewa hivyo. Afida anasema kuwa anajua kuwa huko kulishwa na kunyweshwa kunahitaji kulipwa

".....huku kunyweshwa na kulishwa nako kwa mtindo wa separato kunahitaji kulipwa, si kwa pesa mbali kwa mambo mengine....." uk. 97

#### **4.2.9 Usaliti**

Kuna usaliti pia katika riwaya hii. Wakati Afida alipokuwa katika uwanja wa ndege aliandamana na watu wa ukoo wake ambao walitarajia mara tu atakapofika na kutulia atawaandikia barua ili kuwajulia hali. Pia walitarajia kuwa vitu walivyoagiza wangevipata.Haya hayakuwezekana. Bali na kutowaandikia hata alizopata kutoka motoni hakuzijibu na kama alizijibu ni chache sana.

Katika barua walizomwandikia walimkumbusha kuwa amesaliti ukoo kwa kutotimiza ahadi alizotoa. Walimwambia kuwa hakujua kulipa fadhila kwa kuwa walimlea alipokuwa kinyandu basi ukoo ulitarajia kuwa angeyakumbuka hayo na kufanya alivyo ahidi. kwa ukoo huu,Afida alikuwa amewasaliti.

Afida pia alimsaliti Shabaan mpenziwe. Yeye mwenyewe anahisi vibaya kwa kuwa hakuweza kumpenda Shabaan kama alivyompenda yeye.

Afida ananung'nika kwa kuwa Shabaan anamdai mapenzi na yeye anaamini kuwa mapenzi yao yamemung'unyuka kwa sababu ya umbali uliopo. Afida anasema,``Asiyekuwapo na lake halipo" wakati ambapo Afida ameamua kuwa mapenzi yao yameisha,Shabaan anazidi kuandika barua ili kumkumbusha Afida kuwa hataraji mapenzi yao kukatika eti kwa sababu ako mbali.

"....Afida mpenzi,mwanzo wowote ule unashida .Ukishavuka .....utaniandikia kudhibitisha kudumu kwa mapenzi yetu.



Mimi siamini kwamba mapenzi yetu  
yatafutika kiupuzi hivi." Uk. 65

Afida alipofika peponi alisahau ahadi alizoweka kwa mamake, Bi Sinangoa, Bi Zaina na mwisho mpenziwe Shabaan. Watu hawa wote walikuwa na matumaini makubwa sana lakini Afida aliwasaliti. Aliwasahau kiasi kwamba hata barua hakuwaandikia.

Afida alihisi usaliti pale ambapo walikosana na She-shaiza kwenye klabu. She-shaiza alipomdhalilisha Afida kwa kuwa ni m-Motoni Afida anajitetea kwa kumtukana. Afida alitarajia kuwa Neshboch atamtetea lakini badala yake anamuonya asibishane na Shesha-iza kwa sababu angewakasirisha wapeponi wote.

".....unajua Afi, "Neshboch akaja juu, `bora wewe uteremke matao ya chini tu. Usimjibu She-shaiza, maana majibu yako yanakuwa makali na kuwakata maini ya wapeponi wote." Uk 53

Maneno ya Neshbosh yalimuudhi Afida kwani hangetarajia mumewe kukubaliana na kauli kuwa yeye Afida hakuwa m-Peponi hata kama alikuwa na paspoti na licha ya kuwa mkewe.

"Nashangaa hata wewe Nesh, unajifanya mimi paka'si mtu kamwe....." Uk. 154

Wakili wa Afida pia alimsaliti Afida katika kesi iliyomkabili. Baada ya Afida kushtakiwa kuwa hangeweza kulea kwa sababu alikuwa mlevi, siku za kesi wakili wa Afida hakufika mahakamani kumtetea. Kwa kuwa hangeweza kujitetea kitoto chake kilichukuliwa na Neshboch mumewe. Wakili huyo kulingana na Afida alinunuliwa kwa pesa au kwa mori wa kisiasa. Huu ulikuwa usaliti kwa sababu Afida alitarajia kuwa wakili huyo ndiye angemsaidia lakini hata yeye alimwacha bila mtetezi

Saparato ambaye alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Afida pia alimsaliti. Baada ya kumtia mimba alikataa jukumu la kumlea mtoto. Baada ya Afida kujifungua wanapokutana na Saparato, Saparato anamwambia Afida kuwa wazazi wake hawatamkubali mtoto wa Afida kwa sababu hafanani na wapeponi. Afida anamkumbusha saporato kuwa yeye ni m-Peponi. Saporato anamwambia Afida kuwa hawi m-Peponi kwa sababu ya paspoti tu. Afida hangetarajia kuwa Saporato angemwambia hivyo. Afida anashangazwa sana na maneno ya Saporato na kumuuliza, hata wewe Saporato? Siamini hivyo."

Saparato pia alimsaliti Afida kwa kukataa kumsaidia kulea mtoto ambaye alijua kuwa alikuwa wake.

Maneno yote wanayosemwa na Neshboch ni ya kumuudhi Afida na yanakusudiwa kuonyesha kuwa hata unapopata paspoti ya nchi yao bado hawakutambui. Linaloudhi Afida zaidi ni kuwa hata Neshboch mumewe anamtukana.

Kwa kutumia maneno yanayomuudhi Afida, na zaidi yakisemwa na watu ambao walikuwa na uhusiano wa kimapenzi, mwandishi amefaulu kuonyesha jinsi watu weusi wanavyodharauliwa na wazungu. Matumizi ya maneno yanayouudhi kama wanavyofanya Neshboch na wengine ni ukiushi wa kanuni za upole za Brown na Levinson (1987). Watu wa Peponi wanapooonea na Afida, wnamwonyesha kuwa yeye ni m-Motoni na hawezi kuwa m-Peponi kwa vyovyote vile.

#### **4.2.10 Ubaguzi wa Rangi**

Katika riwaya hii kuna ubaguzi wa rangi. Afida anapofika peponi, baada ya muda anapelekwa katika chuo kikuu ili kupata elimu na pia kusoma lugha ya peponi. Akiwa chuoni walimu na hata wanafunzi wenzake walimbagua. Kulingana na Afida wanafunzi ndio waliokuwa wabaya zaidi.

".....Labda wanafunzi waliokuwa hawawezekani. Walinitenga, wengine walinibagua. Wakadhani kama mimi si mtu ni dude tu, au labda mtu aliyetoka mwezini." Afida alikuwa na shida hata kupata rafiki. Uk. 90

Baada ya Afida kuolewa na Neshboch, dada yake Neshboch alikuwa hampendi Afida kwa sababu alikuwa mmotoni. She-shaiza anasema kuwa si vizuri kwa wa-motoni kupewa paspoti; "Hawa wanaowapa uraia nyinyi hapa Peponi, hata sijui mabwege namna gani wanatoa uraia wan chi takatifu kwa mabwege na vitakataka kama nyinyi. Maneno haya ni matusi kwa Afida anayesimamia jamii ya waafrika. Maneno haya ambayo yamekiuka upole na hivyo yanaudhi na kuaibisha Afida yametumiwa kuonyesha jinsi wazungu wanavyowadharau waafrika na hata hawataki wapewe paspoti.

Wawili hawa wanaendelea kurushiana maneno makali na hata anapoyaingilia Neshboch mumewe Afida, anamtaka Afida anyamaze ili asiwaudhi wa-Peponi wote. Ugomvi huu unazidi mpaka Sheshaiza na Bendelheib nduguye wanataka kupigana. Kwa uchungu wa kutukanwa

Afida anaondoka na kuwaacha.

Ubaguzi unadhihirika hata kwenye vyumba vya starehe. Wakati mmoja Afida anaenda kwenye baa na kuanza kuropokwa maneno kwamba alikuwa anataka kutiwa mimba. Mwenye baa, badala ya kumwambia anyamaze alimtukana kwa kumwambia kuwa yeye ni mwanamke mweusi.

"sharrap, hapa si pahali pa makelele, wewe  
mwamnamke mweusi... hapa si Motoni."  
Uk. 181

Afida alikuwa na machungu kwa kuponyokwa mtoto wake na anapiga kelele na kusema kuwa Peponi hakuna haki kwa wanaoitwa wageni alidhibitisha kuwa wageni walikuwa wanaonewa. Anapoambiwa anyamaze anasema kuwa hatanyamaza bali atasema kuwa wageni hawana haki Peponi.

#### **4.2.11 Udhalilishaji**

Udhalilishaji pia ni maudhui ambayo ni dhahiri katika riwaya hii. Kinyume na matarajio, Bi. Marneti, anamdhalilisha Afida pale anapompeleka hospitali. Anaeleza kuwa mambo ya heater yeye hayaelewi. Anasema kuwa Afida ni mjinga.

Udhalilishaji pia unadhihirika katika mawazo ya Afida. Afida anapoingia kwenye gari anaanza kuwaza jinsi wa-Peponi wanavyowachukulia wa-Motoni. wa-Peponi huchukuliwa ni ukweli mtupu. wao wanaamini kuwa wa motoni ni wajinga.

"Ukiwauliza kwa nini wa-motoni kuwa wa-  
motoni, jibu ni lile, "Wa- Motoni  
hawabadiliki, hata mmoja habadiliki, ni  
wajinga, hawana elimu na ni washenzi." Uk. 64

Afida pia anachukuliwa kuwa wa-peponi huwadhalilisha wa-motoni hata wanapotembea kwao. Anasema kuwa watalii wanapotembea nchi za waafrika hupiga picha wale watu ambao ni maskini, watu ambao kazi yao ni kukaa kando kando ya barabara wakiuza matunda. Picha hizi baadaye zinapofika peponi zinatumiwa kuonyesha jinsi wa-Motoni walivyo maskini na jinsi ambavyo hakuna chochote wanachoelewa ila kubeba visu na kumenya matunda. Picha hizi ndizo huwafanya wa-Peponi kuchukuliwa kwa jumla kuwa wa-Motoni ni wajinga, maskini na hakuna lolote la maana wanalolijua.

Wa-Motoni walidhalilishwa hata kwa misingi ya lugha yao. Afida anaeleza kuwa hata wanapoingia kwenye basi na rafikiye Shuhuda, wa-Peponi huwaangalia kwa mshangao. Wanadai kuwa lugha ya wa-Motoni ni ya kelele na fujo kila siku. Jambo hili linamkera Afida kwa sababu ni kawaida kwa watu kuongea kwa furaha wanapokutana ugenini. Ni kweli kuwa hata hao wa-Peponi wakikutana motoni watafurahi na kushangilia kama wafanyavyo Afida na Shuhuda wakutanapo.

Chuoni alikosomea lugha walimdhaliisha. Kila wakati walimu walikuwa wakimuuliza Afida kama kipeponi ni kigumu. Swali hili lilikuwa linalenga kudhibitisha kuwa wanaozungumza kipeponi wana akili nyingi kuliko watu wengine wote. Wapeponi walichukuliwa kuwa wanaozungumza kipeponi ni werevu zaidi kuliko watu wengine. Ukweli ni kwamba hakuna lugha iliyo juu kuliko nyingine na lugha zote ni sawa. Huu ukweli ndio uliomuumiza Afida kila alipoulizwa kuhusu ugumu wa lugha ya peponi. Alielewa kuwa hata wa-peponi wangepunzwa ki-Motoni wangepunza kigumu.

Afida alikumbana na watu waliomdhailisha hata katika vyumba vya starehe alipokutana na watu waliotaka kujua alikotoka. Afida anadai kuwa wa-Peponi hawaulizi maswali kwa kujua bali kwa udaku na kejeli ndani yake. Anasema kuwa maswali yao huwa ni ya kumdhaliisha na kumkunisha mtu ili ajihisi kwamba yeye si lolote si chochote. Jambo hilo linadhahirika pale wanapokutana na Yakrobich. Katika hali ya kuulizana na kujibiana maswali ili kuweza kujuana Yakrobich anamwambia Afida kuwa anasikia kuwa Motoni hakuna shule wala vyuo vya maana. Anaendelea kusema kuwa watu wa Motoni hawafundishwi vizuri na wala hawasomi kamwe.

Hata kama Afida aliudhika na kauli ya Yakrobich alimjibu kwa upole kuwa angoje wafikapo darasani atayagundua mambo hayo kama ni kweli au si kweli.

Wakati wa harusi ya Afida na Neshboch, She-shaiza anamuuliza maswali ya kipuuzi. Anamuuliza kama motoni kuna vyakula vitamu kama vya peponi na kama Saiwama wanakunywa damu. Afida anayapuuza maswali mengine kwa sababu alijua kwamba yalikuwa ya kumdhaliisha.

Kwa kutumia matusi, mwandishi amefaulu kujenga na kuendeleza maudhui ya udhalilishaji. Tangu Afida afike Peponi, hakukutana na watu ambao walimsaidia kutulia kwa furaha. Mazungumzo yake na watu wa Peponi, hata wale anadhani wanaweza kumsaidia yanamuudhi

kwa sababu wote wanataka kumwonyesha kuwa yeye ni kiumbe duni na hawezi kuwa kama watu wa Peponi. Kulingana na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987), watu wanapozungumza, kila mshiriki anafaa kuhifadhi uso wa mwenzake na asipofanya hivyo basi anakiuka kanuni za upole.

#### **4.2.12 Majuto**

Katika riwaya hii pia kuna wahusika ambao wanajuta vitendo vyao vya awali. Kwanza kabisa Afida mwenyewe anajuta. Anajuta kwa sababu aliwaacha wazazi wake motoni na hakuwajali tena. Hakuwaandikia barua hata moja wazazi wake alipofika peponi. Anajuta kwa kifo cha mpenziwe Shabaan kwa sababu alikufa kwa kumwaza Afida. Anajuta kwa kuvunja ahadi ya mapenzi aliyompa Shabaan. Hata kwenye harusi yake anamkumbuka shabaan na kuwa alijitoa uhai kwa sababu yake. Afida kwa kiasi fulani anajuta kuacha utamaduni wake. Kumbusu mtu na kugandisha midomo kwenye midomo ya mtu mwingine lilikuwa jambo la ajabu katika jamii yake. Anashangaa ni vipi amevunja ahadi aliyojipa mwenyewe. Anajituliza mwenyewe kwa kusema; "ningefanya nini? Unapokuwa mhitaji unakuwa baradhuli."

Majuto ya Afida hayaishii hapo. Baada ya mtoto wake kuchukuliwa, anaingilia ulevi na hawezi tena kujinunulia pombe na pia kumhudumia mtoto wake. Anaingilia maisha ya ukahaba na anayaingilia maisha ya pombe na wanaume. Inafika wakati Afida anaanza kujuta kwa nini alikubali kushawishiwa na Neshboch kunywa pombe, kwa nini alikubali kuolewa naye badala ya kuolewa na kijana mdogo kama Yakrobich. Afida hata aliyajutia maisha yake ya ukahaba. Baada ya Afida kuugua na kupelekwa hospitalini, alijuta hata kuzaliwa.

"Naumia mimi, naumia--- Kwa nini mimi, kwa nini mamangu hakuniua wakati ule alipokwisha nizaa?" "Tafadhali mwambie mamangu anisamehe na mimi namsamehe."  
Uk. 190

Afida anapoongea kwenye simu na Profesa Marjan anamwambia profesa kuwa dunia imemfikisha pabaya na amekosa. Anasema kuwa katika dunia hii ukikosea step moja unaisha kabisa.

Baada ya mazungumzo haya Afida hasikiki tena wala kuonekana. Rafikiye Shuhuda ambaye alikuwa amelazwa hospitalini kwa ugonjwa wa ukimwi pia alikuwa na majuto. Afida anapoenda

kumuona hospitali anamuuliza kwa nini hakumkataza maisha yake yaliyokuwa yamemfikisha hapo. Afida hapa pia ni kama anajuta kuja peponi. Anamwambia shuhuda kuwa labda kama wangebaki motoni shida hizo hazingewapata. Wote wawili wana majuto lakini wanakubaliana kuwa ujana ndio uliowatenda hayo yote.

Mwanzo na mwisho wa riwaya hii una maudhui ya mauti. Wakati Afida alipofika peponi na kumsahau shabaan, shaaban hakuweza kustahimili maisha bila Afida na hivyo akajitoa uhai.

Shuhuda ambaye alimtangulia Afida Peponi anakufa kwa ugonjwa wa ukimwi. Hata kama hatujaambiwa waziwazi, Afida pia anakufa kutokana na ugonjwa wa seratani uliokuwa umelaza hospitali. Riwaya hii inafika kikomo bila kujua alikoenda Afida. Profesa Marjan na mkewe ndio waliokwenda kumtafuta baada ya kuongea naye kwa simu. Hawakumwona lakini walimchukua mtoto wake na kumpeana kwenye kituo cha polisi.

#### **4.3 HITIMISHO**

*Mhanga Nasfsi Yangu* ni riwaya ambayo ina maudhui mengi sana. Kuna maudhui makuu ambayo ni matumaini ambayo yanadhihirishwa na wahusika wajenzi ambao wamemsindikiza Afida kwenda Peponi. Kuna wale ambao wana matumaini kuwa Afida akifika peponi atapata pesa na ataweza kuwafanyia mamabo makubwa makubwa kama vile kuwalipia tiketi wakatibiwe peponi, kuwanunulia mabati ya kukarabati nyumba. Mamake afida ana matumaini kuwa Afida atapata pesa na atamununulia magari makubwa ya kubeba mizigo ya biashara ili atoke kwenye umaskini.

Shabaan ana matumaini kuwa Afida atakapofika peponi hatasahau mapenzi yao na atarudi ili wafunge ndoa. Afida mwenyewe pia ana matumaini kuwa afikapo peponi maisha yatakuwa ni ya raha na hatakuwa na shida yoyote. Ajabu ni kwamba matumaini haya yamebaki kuwa matumaini kwani hakuna yeyote aliyepata alichotumainia.

Kuna maudhui ya maonevu na ubaguzi wa rangi. Afida anapofika peponi anakumbana na hali ambayo hakutarajia. Shangaziye anamchukia na kumtenda vitendo vya unyama. Anamlaza kwenye chumba ambacho hakina mashine ya joto, anamkataza kuoga anapotaka, anamsingizia anamnyemelea mumewe. Bali na hayo anamshawishi Afida aolewe na Neshboch ili wapatao mtoto shangazi yake Marneti amchukue huyo mtoto kwa sababu yeye alikuwa tasa. Chuoni Afida anabaguliwa na wanafunzi wengine kwa kuwa ni m-Motoni. Kwa vilabu pia anabaguliwa

na kutukanwa. Afida anabaguliwa hata na ndugu zake mume kwa kuwa ni mweusi.

Maudhui ya usaliti pia yamo katika riwaya hii. Afida amewasaliti watu wa ukoo wake ambao walitarajia angewasaidia, amemsaliti Shabaan ambaye alitarajia angerudi wafunge ndoa na hata barua zake za mapenzi alikuwa hazijibu.

Afida pia amesalitiwa na watu ambao alifikiria angewaamini. Anapokonywa mtoto, anaweka wakili ambaye anatarajia atamtetea ili apate mtoto wake. Wakili hafiki kortini na hivyo anapokonywa mtoto wake. Afida pia anasalitiwa na mumewe Neshboch pale anapokataa kumtetetea anapotukanwa na Sheshaiza. Afida hatarajii Neshboch amkumbushe kuwa yeye ni mmotoni hata kama ana paspoti. Usaliti mkubwa unatokea pale ambapo Neshboch anapanga njama na wapangaji kumsingizia Afida kuwa ni mlevi na hivyo hawezi kulea mtoto. Kwa misingi hiyo ambayo ilikuwa ni kisingizio Afida anapokonywa mtoto.

Udhalilishaji pia umo katika *Mhanga Nasfsi Yangu*. Afida anadhalilishwa na watu wa peponi akiwepo shangazi yake Bi. Marneti. Shangazi yake anapompeleka hospitali anaambia daktari Afida ni mjinga kwa sababu hajakaa sana peponi. Daktari amwambia Afida kuwa peponi watu hawafi kwa magonjwa mabaya kama vile ukimwi, kifua kikuu na malaria. Anadai kuwa peponi watu hufa tu kwa homa kali. Maisha ya Afida wakati wote yalizingirwa na watu ambao waliwaona watu weusi kama ambao si watu.

Maudhui ya majuto pia yako. Afida na Shuhuda wanajuta kwa sababu ya maisha yao peponi. Wanajuta kwa sababu hawakuweza kuafikia yaliyowaleta peponi.

Kuna maudhui ya uozo wa jamii. Maisha ya starehe ambazo zinaishia kwa mambo mabaya kama vile uasherati. Ufisadi pia unaonekana pale ambapo Afida anapokonywa mtoto. Wakili wa Afida anahongwa ili asifike kortini. Uozo wa jamii unadhihirika pale ambapo Marneti anapanga Afida aolewe na mzee ili wapate mtoto ili naye amchukue.

Wasiwasi pia ni jambo jingine linalojitokeza katika riwaya hii. Afida ana wasiwasi kwa sababu hana uhakika anakoenda, Shabaan ana wasiwasi kwa sababu hakuwa na hakika kuwa Afida angerudi. Hata watu wa ukoo wa Afida walikuwa na wasiwasi hawakuwa na hakika kuwa mambo walioagiza wangepata

Kuna maudhui mengine ambayo hayakujengwa sana kama vile mapenzi, umaskini, uchumi,

chuki na elimu. Maudhui yanayokamilisha riwaya hii ni ya mauti. Shuhuda anaugua ugojwa wa ukimwi na anakufa. Afida naye anakufa kwa ugojwa wa saratani ya tumbo na la kuhuzunisha ni kwamba mtoto wa Afida anaachwa mikononi mwa polisi kwa sababu hakuna mtu ambaye angekaa na yeye. Kifo cha Afida ni kudhaniwa tu kwani baada ya kumpigia profesa simu akiwa na uchungu hakisikika tena.

Kwa jumla riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ni riwaya nzuri ambayo inaweka wazi jinsi watu wanavyofikiria kuhusu maisha ya nchi za ng'ambo. Anaweka wazi dhana potovu ambayo watu huwa nayo kuwa ukienda huko ni lazima ufanikiwe na utajirike upate pesa za kuwapatia uliowaacha.

Kuweza kuweka mambo haya yote wazi, mwandishi amemtumia mhusika mkuu Afida. Watu wa ukoo wake wametumiwa kuonyesha matumaini ambayo watu huwa nayo mtu anapoenda nchi za ulaya. Mawazo ya mwafrika kuwa ugaibuni kuna kila kitu yamewekwa dosari na mwandishi wa riwaya hii S.A. Mohamed. Mwandishi amewatumia Shuhuda na Afida kuonyesha kuwa maisha ya ugaibuni yanaweza kuwa mabaya hata kuliko ya nchi zetu za Afrika.

Kwa mukhtasari tunasema kuwa hii ni riwaya yenye mafunzo na ambayo inaburudisha na mtu anayeisoma anapata dhana mpya ya ugaibuni.



## SURA YA TANO

### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeangazia kwa muhtasari tasnifu yote. Tasnifu hii ina sura nne.

Katika sura ya kwanza tumeweka msingi wa tasnifu nzima kwa kuangalia maswali ya utafiti, njia za utafiti, nadharia tete, sababu ya kuchagua mada hii na yaliyoandikwa kuhusu mada.

Tumeangazia nadharia za upole ambazo tumezitumia katika kuchanganua *Mhanga Nafsi Yangu*. Nadharia tulizozitumia ni nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) na kanuni za upole za Grice (1975).

Katika sura ya pili tumeangalia jinsi ukiushi umetumiwa kujenga maudhui katika riwaya teule. Tumezieleza nadharia hizo na kueleza jinsi ukiushi umetumiwa kuendeleza maudhui katika *Mhanga Nafsi Yangu*.

Katika sura ya tatu, tumeangalia maudhui yote kwa jumla lakini tumeeleza jinsi ukiushi wa upole umetumiwa kujenga na kuendeleza maudhui makuu. Maudhui makuu katika riwaya hii ni udhalilishaji, ubaguzi wa rangi, udunishaji na dhulma. Tumeeleza jinsi maudhui yameendelezwa kwa kutumia ukiushi wa upole kwa misingi ya nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) na kanuni za upole za Grice (1975).

Katika sura ya nne, tumeangazia fani mbalimbali ambazo mwandishi ametumia kuendeleza maudhui katika *Mhanga Nafsi Yangu*. Tumeangalia jinsi ukiushi wa upole umetumiwa kama mtindo ambao mwandishi ametumia kujenga na kuendeleza maudhui.

### 5.1 Matokeo

Utafiti wetu ulikuwa na malengo matatu ambayo ni; kuchunguza kama nadharia ya upole inaweza kutumiwa kuchanganua kazi ya fasihi, kubaini ni wahusika wapi wametumiwa kuendeleza maudhui, kubaini ni mambo gani ambayo yanachochea ukiushi wa upole katika riwaya hii.

Tumbainisha kuwa nadharia ya upole japo ni ya isimu inaweza kutumiwa kuchanganua kazi ya fasihi andishi. Vilevile, tumebainisha kuwa ukiushi wa upole huchochewa na muktatha wa mawasiliano, swala linalojadiliwa na hisia za wanaozungumza. umebainisha kuwa mwandishi

amewatumia wahusika wajenzi kutoa picha kamili ya maisha ya wageni katika nchi za ng`ambo.

## **5.2 Matatizo ya utafiti**

Matatizo ya utafiti huu japo si mengi ni kuwa lugha ya ukiushi ambaayo imetumiwa na mwandishi inaingiliana na lugha ya kawaida. Hata kama mwandishi ametumia matusi na kejeli, inakuwa vigumu kueleza ukiushi umeanzia wapi na kuishia wapi.

Kinachobainishwa na waasisi wa nadharia ya upole kama ukiushi, ni lugha ambayo hutumiwa kawaida na watu wakiwa na hasira au wakiwa na kusudi la kuudhi au kudunisha mtu.

## **5.3 Mapendekezo**

Nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) inamlelea sana msemaji kwani inahimiza kuhifadhi uso wa msikilizaji. Inasema kuwa msemaji anafaa kuwa mwangalifu asiadhiri uso chanya au uso hasi wa msikilizaji. Tungependekeza wataalam wengine waibue nadharia nyingine au waendeleze zilizoko ili kushughulikia msikilizaji. Mawasiliano yanafaa kuendelezwa na watu wawili na wote wawe na majukumu sawa.

## MAREJELEO

- Bell, D. & Youmans, M. (2006). *Politeness and Praise*.
- Brown, P. & Yule, G. (1983). *Discourse analysis*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Buliba, A., Njogu & Mwihaki, A. (2006). *Isimujamii kwa wanafunzi*; Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation
- Coates, J. (1986). *Women, Men and Language*: Essex, Longman group U.K limited.
- David, K. & Thomas (1969) Choice of words.
- Gadzar, G. (1979). *Pragmatics: Implicature, Presupposition and Logical Form*. New York: Academic press.
- Goffman, E. (1959). *The Presentation of self in everyday life*. New York : Double day
- Goffman, E. (1967). *Interaction ritual*. Pantheon
- Grice H. P. (1975). *Logic and conversation. Philosophy of Language*. New York, NY: Oxford University Press.
- Guiner, L. (1998). *Life as a Female Gentleman in exploring language na Goshgarian 8<sup>th</sup> edition*. U.S: Addison. Wesley Education publisher inc.
- Henrik karsberg. (2012). *Politeness Strategies - A Theoretical framework, Social Linguistic & Observations of politeness*.
- Habwe, J. H. (1999). A discourse Analysis of Swahili political discourse. Unpublished PhD thesis. Kenya: University of Nairobi.
- Habwe, J. H. (2010). Dialogue Drama in Kenyan political speeches and its Pragmatics implications. Kenya: University of Nairobi. *Nordic Journal of African studies 19(3): pp 165-180*.
- Habwe, J. H. (2010). Politness Phenomena: A case of Kiswahili honorifics. Kenya: University of Nairobi. *Swahili forum 17 (2010): pp 126 - 142*
- Izard, C. (1969). *The Face of Emotion*: New York: Appleton. Century Crofts. Jomo Kenyatta
- Johnstone, B. (2008). *Discourse analysis*. Meldon, MA, USA: Blackwell publishers.
- Juez. (1994). *Irony and Politeness*. Los Angeles.
- Lackoff, R. (1976). *Language and society in a survey of Applied Linguistics*. University of Michigan Press
- Leech, G. (1983). *Principles of politeness*. London: Longman
- Levinson & Brown. (1987). *Some universals in politeness usage*: Cambridge University Press

Mohamed, S. A. (2012). *Mhanga Nafsi Yangu*. Longhorn publishers.

Thonus, T. (1999). *How to communicate politely and be a tutor too*.

White L. (1959). *The concept of culture*. U.S.A: American Anthropologists.